Jumanne Mei 18, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580584

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**Mwinyi:** UDSM walinivunjia heshima, pia awataja wanafunzi wa SUA, Muhimbili

UKURASA 3



**Majaliwa** aagiza machinjio Vingunguti kuanza kutumika

UKURASA 5




**Haaland kubakia Dortmund msimu ujao**

UKURASA 20

## TATHMINI COVID-19

# Kamati yabaini chanjo corona zina ufanisi

• **Yatoa** mapendekezo 19, yashauri serikali itoe taarifa ya uwapo wa ugonjwa... *Endelea ukurasa 2*

- Matumizi huru chanjo corona
- Mipango ya dharura kukabiliana na majanga
- Tanzania itekeleze maazimio ya kikanda, kimataifa
- Uanzishaji viwanda vya kutengeneza chanjo
- Utolewaji taarifa sahihi za ugonjwa wa corona
- Matumizi tiba asili, yazingatie misingi ya kisayansi
- Wazee, wenye maradhi sugu wapewe kipaumbele



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea ripoti ya Kamati Maalum aliyoiunda kwa ajili ya kufanya tathmini ya ugonjwa wa COVID- 19 kwa Mwenyekiti wa kamati hiyo, Prof. Said Avoid, Ikulu, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: IKULU**

## Kilio cha wabunge ujenzi barabara chatawala bungeni

UKURASA 8

## Samia: Majaji katendeni haki

UK. 8

**MICHEZO** **YANGA, SIMBA ZATOA NENO KUVAANA JULAI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

TATHMINI COVID-19

# Kamati yatoa mapendekezo 19



Kamati maalum ya kutathmini hali ya corona nchini ikiwasilisha ripoti kwa Rais Samia Suluhu Hassan. **NA MPIGAPICHA WETU**

**Na Christina Mwakangale**

KAMATI ya kitaalamu iliyoundwa kufanya tathmini ya hali ya ugonjwa wa corona nchini, imetoa mapendekezo 19 ikiwamo matumizi huru ya chanjo ya ugonjwa huo, ili kutoa fursa ya kinga kwa makundi maalumu kama wazee, wenye magonjwa sugu na wahudumu wa afya.

Kamati hiyo pia imebaini kuwa chanjo hizo zina ufanisi na usalama unaokubalika kisayansi na kwamba kabla ya kutolewa kwa makundi hayo kwanza zifanyiwe uchunguzi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Prof. Said Aboud, akikabidhi ripoti ya kamati hiyo jana kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu, jijini Dar es Salaam, alisema chanjo zilizoorodheshwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) ziruhusiwe kwa makundi maalumu.

Profesa Aboud alisema: "Pamoja na mapendekezo haya, Kamati Huru ya Kitaifa ya Ushauri wa Chanjo (NITAG) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), ziendelee kushirikishwa katika kutoa ushauri na kudhibiti chanjo hizo."

Aliongeza: "Watu walio na hatari ya kupata maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona wapewe fursa ya kupatiwa chanjo hiyo."

Rais Samia alitangaza kuunda kamati hiyo Aprili 6, mwaka huu ikiwa ni wiki chache baada ya kuapishwa, huku msisitizo mkubwa ukiwa katika kupambana na ugonjwa huo kwa njia za kisayansi.

Prof. Aboud alisema kamati hiyo ilifanyia kazi hadidu za rejea 12, zilizohusu maeneo mbalimbali ya tathmini ya mwenendo wa ugonjwa pamoja na afua za udhibiti ikiwamo chanjo hapa nchini, kikanda na kimataifa.


"Tangu kuingia kwa ugonjwa wa corona nchini Machi mwaka jana, Tanzania imekumbwa na mawimbi mawili makubwa. Na hivi sasa kutokana na mwenendo wa ugonjwa katika mataifa mengine duniani kuna tishio la kutokea kwa wimbi la tatu hapa nchini," alisema Prof. Aboud.

Alibainisha kwamba baada ya uchambuzi uliofanywa na kamati, mapendekezo kwa serikali ni kuihuisha mipango ya dharura katika ngazi zote, kwa ajili ya kukabiliana na majanga ikiwamo ugonjwa wa corona.

Prof. Aboud alibainisha kwamba, kamati imependekeza serikali itoe taarifa juu ya uwapo wa ugonjwa huo, ichukue hatua madhubuti kuimarisha hatua zote za afua za kinga ili kuepusha wimbi la tatu la ugonjwa huo.

Alisema pendekezo lingine ni wataalamu wa afya watimize wajibu wao kitaalamu, kwa kuzingatia weledi, miiko na maadili katika kuelimisha, kukinga na kutibu ugonjwa huo nchini.

Lingine ni Tanzania ishiriki ipasavyo katika maamuzi na itekeleze maazimio ya kikanda na kimataifa, iliyoridhia katika Jumuiya za Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Afrika (AU) pamoja na Shirika la Afya Duniani (WHO).



kuhusu matumizi ya chanjo, Prof. Aboud alisema kamati inashauri kwamba serikali kutumia vyombo vyake na kuendelea kuchukua hatua kuelekea kuruhusu matumizi huru ya chanjo.

"Kipaumbele cha utoaji wa chanjo dhidi ya corona nchini kwa kuanzia kiwe katika makundi muhimu, wahudumu katika vituo vya kutolea huduma za afya na watumishi walio katika mstari wa mbele wa utoaji wa huduma, mathalani watumishi sekta ya utalii, hoteli, mipakani, viongozi wa dini na mahujaji.

"Wazee na watu wazima kuanzia umri wa miaka zaidi ya 50, wenye maradhi sugu, kisukari, shinikizo la damu, maradhi ya mfumo wa upumuaji, magonjwa ya figo," alisema Prof. Aboud.

Pia Prof. Aboud alisema kamati pia inapendekeza chanjo hiyo ipewe kipaumbele kwa watumishi wa vyombo vya ulinzi na usalama, wasafiri wanaokwenda nje ya nchi.

Alisema hivi sasa ufanyike uhamasishaji na maandalizi ya upokeaji, utunzaji, usafirishaji na utoaji wa chanjo nchini na wananchi kuwa huru kuamua kuchanja ama la.

"Serikali iratibu upatikanaji wa chanjo kwa watumishi wa taasisi za kimataifa walioko nchini, ijiunge na 'COVAX Facility' kwa kuwasilisha andiko la kupatiwa chanjo, kwa kutumia fursa inayotolewa na GAVI."

"Serikali itumie fursa zilizopo wakati huu wa corona kuanza mchakato wa uanzishaji wa viwanda vya kutengeneza chanjo, iimarishe huduma za uchunguzi kwa kuijengea uwezo Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii na maabara nyingine ili kupanua wigo wa upimaji wa ugonjwa," alisema Prof. Aboud.

Prof. Aboud alisema kamati inapendekeza serikali kujenga uwezo wa ndani wa utambuzi wa virusi anuai vinavyosababisha ugonjwa wa corona na magonjwa mengine ya kuambukiza.

Alisema serikali pia itoe takwimu sahihi za ugonjwa wa corona kwa umma na WHO, ili wananchi wapate taarifa sahihi kutoka mamlaka za serikali na kuheshimu makubaliano na kanuni ambazo nchi iliridhia.

Mwenyekiti huyo alisema kamati inapendekeza kuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ikamilisha mwongozo mpya wa matibabu ya ugonjwa huo.

"Serikali iendelee kuhakikisha kuwa matumizi ya tiba asili na tiba mbadala katika mfumo rasmi wa tiba za kisasa yanazingatia misingi ya kisayansi.

"Na serikali iendelee kutoa fursa na kuwawezesha wanasayansi kufanya utafiti kwa kufuata miiko, maadili na taratibu zilizowekwa ili kuimarisha kinga, tiba, uchunguzi wa ugonjwa wa corona na athari zake katika jamii nchini," alisema Prof. Aboud.

Pia alisema kamati inapendekeza serikali kuendelea kuzingatia mazingira ya Kitanzania katika udhibiti wa corona katika kuamua kuweka au kutokuweka shuruti ya kujifungia na kuwa na ubunifu, ili kuruhusu ukuaji wa uchumi na kuimarisha sekta zinazochangia katika uchumi.

"Wizara yenye dhamana ya fedha na uchumi ifanye tathmini ya kina ya athari za corona na kuweka mpango madhubuti wa haraka wa sasa, wa muda wa kati na muda mrefu unaotekelezeka, ili kukuza uchumi wa nchi."

"Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ziendelee kushirikiana ipasavyo katika hatua zote za kukabiliana na corona pamoja na majanga mengineyo ikiwemo utoaji wa nyaraka za kimataifa kama vile tahadhari ya kusafiri," alisema Prof. Aboud.

Alisema Idara ya Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, iendelee kutekeleza ipasavyo jukumu la uratibu na kutoa rasilimali husika, wakati wa majanga ya kitaifa na kimataifa kama ugonjwa huo kwa kushirikisha ngazi na sekta zote.

Pia serikali ikamilishe malipo ya madeni ya watoa huduma na watumishi waliokuwa mstari wa mbele katika kukabiliana na ugonjwa huo, ili kuongeza ari na tija ya udhibiti wa ugonjwa huo.

Pendekezo lingine ni serikali iendelee kushirikisha wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini, wadau wa maendeleo, sekta binafsi na vyombo vya habari katika mapambano dhidi ya corona.

## HABARI KITAIFA

## Corona ilivyoathiri usafirishaji bandarini

**Salome Kitomari**, DODOMA

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi imesema janga la corona limesababisha athari ya mapato na kupungua kwa abiria, mizigo kwenye usafiri wa anga na shehena inayoshushwa bandarini.

Pia idadi ya wasafiri wa anga ilipungua kutoka 4,423,7332 hadi 2,495,379. Akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo, Dk. Leonard Chamuriho, alisema katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, idadi ya abiria wanaotumia usafiri wa anga imepungua na kufikia 2,495,379 ikilinganishwa na abiria 4,423,732 waliotumia usafiri huo katika kipindi cha 2019/2020.

Alisema upungufu huo ni sawa na asilimia 43, na katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, idadi ya abiria wanaosafiri ndani ya nchi imepungua hadi abiria 1,676,107 ikilinganishwa na 2,342,059 waliosafiri katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020.

Kuhusu mizigo, Waziri Chamuriho alisema katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, mizigo iliyosafirishwa ni tani 19,779 ikilinganishwa na tani 20,417 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020, ikiwa ni upungufu wa sawa na asilimia 3.1.

Alisema katika kipindi hicho, miruko ya safari za ndege imeshuka hadi 103,110 kutoka 175,567 ya mwaka 2019/2020, ikiwa ni upungufu wa miruko kwa asilimia 41.3. Kushuka kwa usafirishaji wa abiria, mizigo na miruko ya ndege ni kutokana na athari za corona duniani.



Mkuu wa Kitengo cha Ubunifu na Maendeleo wa Benki ya NMB, Josina Njambi, akiongea na waandishi wa habari (hapo pichani) wakati wa ufunguzi rasmi wa tamasha la Wiki ya Ubunifu iliyoanzishwa na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, Benki ya NMB ni mdhamini wa wiki hiyo ya ubunifu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi: UDSM walinivunjia heshima

- Pia awataja wanafunzi wa SUA, Muhimbili

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, ameutaja mgomo wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) wa Mei 1990 kuwa miongoni mwa vikwazo vilivyoukabili uongozi wake.

Katika kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anasema wanafunzi hao walimvunjia heshima kutokana na kutumia lugha ya matusi dhidi yake binafsi na serikali.

Anasema wanafunzi hao walikuwa na malalamiko yao; wakaamua kuacha kusoma na wakaanza walichokiita 'baraza', lengo lao likiwa waungane, wakubaliane, wawe na msimamo mmoja na wahamasishane kwa hatua walizozikusudia kuchukua dhidi ya serikali.

"Baadhi ya malalamiko yao yalihusu walichokiita kudhibitiwa kwa chama chao cha wanafunzi na tawi la Umoja wa Vijana wa CCM chuoni hapo; kupungua kwa bajeti ya elimu; uhaba wa nafasi, vitabu na huduma za afya; na kupungua kwa uwezo wa posho waliyokuwa wanalipwa kununua mahitaji yao.

"Wakachaguana wachache waje kuniona na kuniletea rasmi mwaliko niende chuoni kusikiliza malalamiko yao. Nikawaambia nitakuja baada ya safari yangu ya nje ya nchi. Hawakuridhika; wakaendelea kugoma.

"Ikabidi serikali itoe karipio kali na kuwataka warejee madarasani vinginevyo hatua kali zingechukuliwa dhidi ya wanaokaidi. Madarasa yakarejea, lakini vurugu nazo zikaendelea, ikiwamo kubandikwa kwa karatasi kwenye mbao za matangazo na maeneo mengine zikiwa na matusi ya kila aina dhidi yangu binafsi na serikali.

"Kwa kweli wanafunzi wale walinivunjia heshima kiasi ambacho hata mtu mvumilivu kama mimi nilishindwa kuendelea kuwavumilia. Hata niliporejea kutoka safari sikwenda kuzungumza nao.

"Mei 12, 1990 ililazimu nikifunge Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kikaja kufunguliwa Januari 1991. Nikawarudisha baadhi ya wanafunzi waliofukuzwa ili wamalize masomo yao.

"Hata hivyo, wanafunzi 13 hawakuruhusiwa kurejea kwa vile ndio walithibitika kuwa vinara wa fujo zilizosababisha chuo kufungwa. Hata hivyo, tuliwaruhusu kuomba kurejeshwa baada ya kutumikia adhabu ya mwaka mmoja nje ya chuo," anasimulia.

Mwinyi anataja mgomo mwingine wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) mkoani Morogoro, ambao wanafunzi walipinga agizo la serikali la kuwataka walale watatu kwa kila chumba kutokana na uhaba wa hosteli.

"Waheshimiwa wale wakaona wamefedheheshwa sana kutakiwa wachangie chumba wanafunzi watatu, japo hatua ile ilikuwa ya muda tu wakati wakisubiri hosteli mpya ikamilike.

"Wanafunzi wale wakakataa, wakagoma na wakafanya fujo kubwa. Ikabidi tuwasimamishe masomo na kuwarejesha makwao wanafunzi 297 kati ya wanafunzi 500 waliokuwapo chuoni hapo enzi hizo," anasema.

Mwinyi anasema mgomo wa tatu wa wanafunzi uliomtikisa ni wa mwanzoni mwa mwaka 1992 uliowahusisha wanafunzi wa udaktari 76 waliokuwa wakifanya kazi chini ya uangalizi wa walimu wao kule Muhimbili.

Anasema mgomo huo ulikuwa mgumu kuumaliza kwa kuwa hata walipochukua hatua ya kuwafukuza, waliungwa mkono na wanataaluma wengine wa Sekta ya Afya na hata wanafunzi wa UDSM.

"Baada ya majadiliano marefu mwafaka ukafikiwa. Kwa ridhaa yangu waliofukuzwa wakarejeshwa kazini na tukaunda kamati chini ya uenyekiti wa ofisi yangu kujadili na hatimaye kumaliza kadhia hiyo. Hadi kufikia Februari 2, 1992 hali ya utulivu ikapatikana," anasimulia.

Kwa mujibu wa Mwinyi, wanafunzi wa udaktari walikuwa na malalamiko kadhaa, yakiwamo madai ya posho mbalimbali walizoona wanapunjwa.

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATRHI**
**MIRATHI NA 32 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**Bernard Lucas Mungwe**
**Mwombaji/waombaji**
**Florence D. Luhasia and Mwinga Bernard**
**Taarifa ya kawaida**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji /mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 1 mwezi wa 6 2021

**Imewasilishwa Dar Es Salaam leo tarehe 3 mwezi 5 2021**

NAIBU MSAJILI

**VEHICLES SALES**

Arysta LifeScience Tanzania is advertising the sale of one company vehicle located in Dodoma. All interested buyers are welcome to view the vehicle at the following location.

1. Dodoma- Nzuguni (10 km from Dodoma city centre)

Type: Nissan
Model: Hard Body (Double Cabin)
Colour: White

**Contacts:**
**+255 744 529 070;**
**+255 762 535 410**

# RPC: Uchunguzi wa awali waliouawa Hifadhi ya Ruaha wameshambuliwa na wanyama

**Na Mwandishi Wetu**

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Mbeya (RPC), Ulrich Matei, amesema watu watatu wanaodaiwa kuingia kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Aprili 23, 2021 kufanya ujangili wa kuvua samaki, wameuawa na wanyama wakali.

Wakati Kamanda Matei akitoa kauli hiyo, Mbunge wa Mbarali, Francis Mtega, ametoa hoja bungeni akisema watu hao wameuawa na askari wa hifadhi.

Kwa upande wake, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema askari wawili wa hifadhi hiyo wanashikiliwa na polisi kwa uchunguzi wa tuhuma hizo.

Kamanda Matei alisema waliouawa na wanyama wakali ni William Estoberi Nundu (38), aliyeliwa na mamba kiwiliwili chake na kubaki kichwa kilichokutwa na majeraha kadhaa.

Mwingine ni Sandu Masanja (28), aliyekutwa amelala kifudifudi kwenye korongo la maji, huku shingo ikiwa inachezacheza na wa tatu ni Ngusa Salawa (14) wa Madabaga, ambaye alikutwa amelala kifudifudi kwenye dimbwi la maji.

Kamanda Matei alisema vifo vya watu hao ambao miili yao ilikutwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha wilayani Mbarali, vilitokana na kushambuliwa na wanyama wakali.




Kamanda wa Polisi Mbeya, Ulrich Matei. **PICHA: MTANDAO**

Alipoulizwa kuhusu kuwapo taarifa katika mitandao ya kijamii zinazodai kuwa watu hao wameuawa na askari wa wanyamapori wanaodhibiti ujangili, Afande Matei alisema:

"Kwenye mitandao ya kijamii mtu yeyote anaweza kusema chochote. Mwenye taarifa sahihi, apeleke ripoti kwenye authority (mamlaka).

"Apeleke kwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, au Kamanda wa Polisi wa Mkoa. Mimi sijapata mtu wa kuniambia kuna moja, mbili, tatu, zaidi ya hiki nilichokwenda kuonyeshwa kilomita 10 kutoka kwenye makazi ya watu; tulikokuta miili inazagaa kwenye maji.

"Tunawashauri wananchi waache kuingia kwenye hifadhi. Humo ndani siyo salama na hasa nyakati hizi za mvua. Ni maeneo hatari kwa maisha yao. Nasema lile eneo, waliosema kuna mamba, wala si mtu mwingine, ni wale wale wanakijiji! Wametuambia kuwa hili eneo lina mamba wengi sana.

"Sasa ukiangalia walivyo-chop (kata) kile kichwa na kuondoa kiwiliwili! Kulikuwa kuna haja ya kukata kichwa hata kama kulikuwa kuna ugomvi na mtu yeyote? Hapana. Ni mnyama mkali ameamua kuchukua ule mwili,

> **"Yalitokea mauaji ya wananchi watatu yaliyotekelezwa na wanaodhaniwa kuwa ni askari wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, TANAPA.**

kaukata...

"Inawezekana akawa amekatwa na mnyama mkali kwa sababu lile eneo lina wanyama wengi sana. Kuna viboko na wanyama kama mamba.

"Lakini tutoe rai, eneo tunaloambiwa ni hifadhi ya taifa, liko protected (limehifadhiwa), tusiende kule. Kikikupata cha kukupata, usimlaumu mtu kwamba hatujakulinda. Maana kazi yetu sisi polisi ni kukulinda wewe Mtanzania. Sasa wewe kama unajiingilia mahala bila hata mtu wa kukusaidia, mwishowe utamlaumu nani?"

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbarali, Telesphor Sambi, katika uchunguzi alioufanyia mwili wa William Estoberi Ngusa, Aprili 27, 2021, unaonyesha kuwa: "Kichwa chake kilikuwa na matundu manne (yanayoaminiwa kuwa ya meno ya mamba) katika pande zote mbili za kichwa kulia na kushoto (hayaingiliani). Matundu mengine manne yalikutwa kwenye ngozi na matundu matatu kwenye fuvu, yaliyotoboa hadi ubongo."

Ripoti ya daktari inaonyesha kuwa Sandu Masanja na Ngusa Salawa, walikufa kwa kuzamishwa kwenye maji (na mamba) na kukosa hewa hadi kupoteza maisha.

Mbunge wa Mbarali, Francis Mtega, wiki iliyopita alitoa hoja bungeni akitaka ufanyike uchunguzi maalumu, akisema watu hao wameuawa na askari wanyamapori katika kijiji cha Nyeregete, Kata ya Lujewa, Jimbo la Mbarali.

"Yalitokea mauaji ya wananchi watatu yaliyotekelezwa na wanaodhaniwa kuwa ni askari wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, TANAPA," alisema.

Pia alisema kuna wananchi wengine watatu hadi sasa hawajapatikana, na walikuwa pamoja na hao waliokufa. Aliwataja kuwa ni Abdallah Dimon, Mussa Ndikwega na Abeid Stephen Obama.

"Ingekuwa ni majangili, wana AK47; that could have been reasonable (hiyo ingefikirika)! Lakini hawana silaha yoyote, wanauawa kikatili," alisema Mtega.

Kadhalika, alisema kuna mgogoro wa mpaka kati ya hifadhi na wananchi ulioanza wakati wa upimaji wa tatu mpaka kwa tangazo la serikali; GN No. 28.

"Mpaka wa kwanza haukuwa na tatizo. Wa pili ulishirikisha wananchi, ila wa tatu haukuwashirikisha wananchi. Vigingi vikawekwa hadi kwenye makazi ya watu katika vijiji kama Ikoga. Mwaka 2016 waliomba mipaka iainishwe, ambapo vijijini zaidi ya 30 viliingizwa kwenye hifadhi," anasema.

"Hii ni kwa sababu tembo wakiingia (vijijini) huswagwa, hakuna tembo anayejeruhiwa hata mguu! Lakini wananchi wanaovua samaki hifadhini, wanauawa!" Alilalamika.

Alimwomba Waziri wa Maliasili na Utalii afanye ziara kwenye eneo la mauaji akawasikilize wananchi na kuwafariji.

Alipoulizwa kuhusu kadhia hiyo, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Chalamila, alisema: "Chanzo changu kikuu cha taarifa ni RPC, na vyombo vingine. Anayetoa taarifa hapo ni RPC. Ananiwakilisha mimi kutoa taarifa hiyo. Vifo vipo ndani ya hifadhi, waliohusika watafahamika. Hali ni salama.

"Jambo la pili, hakuna sheria inayomtaka ofisa yeyote wa hifadhi kumuua mtu, isipokuwa kama tu kulikuwa na mazingira magumu na makubwa ya kihalifu, kigaidi na kivita.

"Hii pia si sababu kwamba kwa kuwa (maiti) wamepatikana ndani ya hifadhi, basi watu wa hifadhi ndio wamefanya hayo. La hasha. Uongozi wa hifadhi utatusaidia katika kupeleleza maana hayo yametokea kwao.

"Kwa sasa nasubiri taarifa kutoka kwa RPC, RCO na Mwendesha Mashtaka, ambao wamelifanyia kazi suala hili kwa kina, watupe mrejesho ili kuwa na taarifa za kina zitakazo niwezesha kuzungumza kwa data bila kuonea mtu."

Gazeti hili lilipomtafuta Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge, Mussa Azzan Zungu, amejibu kwa ufupi: "Subiri taarifa rasmi tafadhali."

Naye Kamishna Msaidizi Mwandamizi Mawasiliano wa TANAPA, Pascal Shelutete, alisema kuwa jambo hilo kwa sasa liko mikononi mwa vyombo vya dola.

Hata hivyo, amesisitiza unuhimu wa wananchi kuheshimu mipaka ya hifadhi, kwa kufanya hivyo watajikinga pia na wanyama wakali waliomo ndani ya maeneo ya hifadhi.

Kulingana na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Maji wa Mwaka 2007/08, mito kama Angasada na mingine, inachangia asilimia 15 ya maji ya Mto Ruaha, ambao ni chanzo kikuu cha maji katika Bwawa la Nyerere (Stiegler's Gorge) linalotarajiwa kuzalisha megawati 2,015 za umeme utakapokamilika.

# Mbaroni akituhumiwa kusafirisha bangi kilo 19

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma linamshikilia, Joseph Komba (35), kwa tuhuma za kusafirisha bangi yenye uzito wa kilo 19.6 kutoka Songea mjini kwenda Mbeya.

Akizungumza na Nipashe jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alisema tukio hilo lilitokea Mei 16, mwaka huu, majira ya saa tano asubuhi katika maeneo ya Mizani nje kidogo ya Manispaa ya Songea.

Alisema askari polisi wakiwa doria walipata taarifa kutoka kwa raia wema kuwa kuna mtu ana mzigo kwenye basi la abiria, ambao ni haramu.

Kamanda Maigwa alifafanua kuwa polisi walianza kumsaka mtuhumiwa huyo na baadaye walimkamata akiwa kwenye gari lenye namba ya usajili T 818 CKR aina ya Yutong, la kusafirisha abiria toka Songea kwenda Tunduma.

Alisema mtuhumiwa aliuficha mzigo wa bangi kwenye mfuko wa sulphate maarufu kama 'shangazi kaja' na kwenye begi dogo la mgongoni lililokuwa limesheheni dawa za kulevya na baada ya mahojiano ya awali, mtuhumiwa alisema alikuwa anatoka Songea kuelekea Mbeya ambako kuna biashara ya aina hiyo.

Kamanda Maigwa ameonya watu wanaojihusisha na biashara ya aina hiyo kuacha kwa kuwa Jeshi la Polisi limejipanga kumshughulikia mtu yeyote atakayekiuka maelekezo hayo kwa mujibu wa sheria za nchi na pia amewaomba wananchi waendelee kushirikiana na polisi kwa kutoa taarifa za uhalifu kwenye maeneo yao.



Balozi wa Ujerumani nchini, Regine Hess akibadilishana hati za makubaliano na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Peter Mathuki, baada ya kutia saini mkataba wa Euro milioni 53.8 zilizotolewa na Ujerumani kusaidia jumuiya hiyo jijini Arusha jana. **PICHA: ASIRAJ MVUNGI**

# Majaliwa aagiza machinjio Vingunguti kuanza kutumika

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), kukamilisha ujenzi wa machinjio ya kisasa, Vingunguti jijini Dar es Salaam.

Alitoa agizo hilo jana alipotembelea mradi wa machinjio hayo.

"Mstahiki Meya na Mkurugenzi, tunahitaji machinjio haya ili tuweze kuanza kazi, lakini jiji na ushiriki wa wafanyabiashara mifugo zungumzeni kila siku ili mfikie hatua kwamba lini muanze, tunataka tuondoke kwenye eneo hili la zamani, kamilisheni hizo asilimia tano zilizobaki."

Alisema mpaka sasa asilimia 95 ya ujenzi wa mradi huo imekamilika ikiwamo mitambo ya kuchinjia na eneo la majitaka wakati tangi la kuhifadhia maji, chumba baridi cha kuhifadhia nyama na kuweka sakafu eneo la nje ya kiwanda na mpaka kufikia Juni 30, 2021 kazi zote zitakuwa zimekamilika.

Kadhalika, Waziri Mkuu ameuagiza uongozi wa Jiji la Dar es Salaam kuhakikisha mifereji ya majitaka yanayotoka katika machinjio hayo yaelekezwe kwenye mifereji maalum hadi mtoni ili yasiingie kwenye makazi ya watu.

Pia amesema ni vyema wafanyabiashara wakaanza kutumia machinjio hayo ya kisasa na yeyote anayetaka kutumia aruhusiwe, "mitambo ipo tayari, ni vyema tukawazoesha ili muweze kujua taratibu, mwenyekiti unaweza kuwa unaandaa baadhi ya ng'ombe wakawa wanakuja kwenye machinjio mapya."

Waziri Mkuu pia amemwagiza Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam kukamilisha haraka taratibu za ujenzi wa sehemu ya reli inayoingia katika machinjio hayo kwa ajili ya kushusha ng'ombe.

"Tunataka tuwe na reli fupi inayoingia hapa kwa ajili ya kushusha ng'ombe, hili lifanyike kwa haraka, kusanya fedha ndani ya jiji, safisha eneo hili na tuwape Shirika la Reli watujengee tawi la kuingia hapa, huu ni mradi mkubwa."

Aliwaasa wafanyabiashara hao kuacha kupiga mihuri ya moto mifugo ili kuifanya ngozi kuwa na thamani. "Ngozi yoyote ile ikiwekwa alama huwa inapoteza thamani, tuelimishane ili tuache kuchora mifugo yetu."

Akizungumzia ujenzi wa mradi huo ambao umefikia asilimia 95, Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam Jumanne Shauri, alisema utagharimu Sh. milioni 12.49 utakapokamilika na utasaidia kupanua wigo wa masoko ya nje na kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na ng'ombe na mbuzi.

# Idris, mwenzake waachiwa huru

**Na Hellen Mwango**

MSANII wa vichekesho, Idris Sultani na mwenzake, wameachiwa huru na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, baada ya upande wa Jamhuri kushindwa kuita mashahidi dhidi ya washtakiwa.

Hatua hiyo imefikiwa jana wakati kesi hiyo ilipopangwa kwa ajili ya kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashid Chaungu.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kusikilizwa, lakini hawakuwa na shahidi.

Hakimu Chaungu alisema upande wa Jamhuri hawana sababu ya msingi ya kutoita shahidi hata kama kesi hiyo ilipangwa kusikilizwa Mei 14, mwaka huu, siku ya Sikukuu ya Eid.

"Februari 22, mwaka huu nilitoa ahirisho la mwisho kwa kesi hii kwa sababu upande wa Jamhuri haukuwa na shahidi, Aprili 29, mwaka huu hakuna shahidi aliyeletwa nikatoa ahirisho jingine la mwisho mpaka leo (jana) bado mmeshindwa kuita mashahidi," alihoji hakimu na kuongeza.

"Kutokana na mazingira haya mahakama yangu inafuta mashtaka dhidi ya washtakiwa, inawaachia huru chini ya kifungu cha 225 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai," alisema Hakimu Chaungu.

Washtakiwa hao waliwekwa chini ya ulinzi wa askari polisi na kuwekwa mahabusu ya mahakama hiyo.

Awali, kabla ya kesi hiyo, Wakili wa Serikali, Silvia Mitanto, aliiambia mahakama kuwa, wameshindwa kupata shahidi jana kwa kuwa kesi hiyo ilipangwa kusikilizwa Mei 14, ambayo ilikuwa sikukuu na kuomba wapangiwe tarehe nyingine.

Mbali na Idris mshtakiwa mwingine katika kesi hiyo ni Innocent Maiga, aliyekuwa akikabiliwa na kosa la kushindwa kutoa taarifa ya mabadiliko ya matumizi ya laini ya simu kwa mtoa leseni, kosa analodaiwa kulitenda kati ya Desemba 1, 2019 na Mei 19, 2020 katika eneo la Mbezi Beach Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam.


**GSP AUCTION MART**

*P.o.Box 31088 Dar es Salaam*
*Tanzania, Tel: + 255 687 638679 +255 654 922892*
*Sinza Africasana near by sokoni Africasana Block No. 31*
*Email: gsp.recovering@gmail.com / gsp.recovering@outlook.com*

KUMB No. AFCL/2021/DM/021

GSP AUCTION MART Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na kampuni ya ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED S.L.P 40780 Dar es salaam tunapenda kutangaza mnada wa hadhara wa kuuza Magari kwa njia ya mnada wa magari twaja hapo chini.Siku ya Jumatatu ya tarehe 31/05/2021 mnada utaanza Saa 5:00 kamili asubuhi katika yadi ya ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED iliyopo Dar es salaam vingunguti na Mwanza Sinai Mabatini.

| CUSTOMER NAME | MODEL | VEH_NO | LOCATION |
|---|---|---|---|
| MOSES PETER ABDONI | LP 909 BUS | T877 DNN | DAR ES SALAAM |
| ABDALLAH KIBWANA KIBWANA | LP 909 BUS | T351 DPS | MWANZA |
| BASHIR LEONI MSIMBE | LP 909 BUS | T163 DNT | DAR ES SALAAM |
| BASHIR LEONI MSIMBE | LP 909 BUS | T164 DNT | DAR ES SALAAM |
| LUKE ASSOCIATE LTD | PRIMA 2523 | T678 DNE | DAR ES SALAAM |
| LUKE ASSOCIATE LTD | PRIMA 2523 | T613 DMQ | DAR ES SALAAM |
| SHABAN RAJABU SOUD | LP 909 BUS | T615 DQF | DAR ES SALAAM |

1. Dhamana itauzwa Kama ilivyo.
2. Mnunuzi anatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki ni juu ya mnunuzi.
5. Kwa yeyote atakayeharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:**
**GSP AUCTION MART PO BOX 310088 DAE ES SALAAM.**
**+255 654 922 892, +255 687 638 679**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wakuu wapya onyesheni uadilifu, hofu ya Mungu

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, ameendelea kupanga safu ya uongozi wa chama na serikali kwa kusuka timu anayotaka kushirikiana nayo katika awamu ya sita ya uongozi wake, safari hii akiteua wakuu wapya wa mikoa na wa taasisi nyingine mbalimbali za umma.

Miongoni mwa wateule ni wakuu wa mikoa, ambao wengi wao wameachwa japo amewabadilishia vituo vya kazi, hata hivyo, ameteua wapya wanaoziba nafasi za wastaafu wakiwamo wa Mkoa ya Kilimanjaro. Tunaamini kuwa wateule waliobakia kwenye nafasi zao na wale wapya walioteuliwa ni wazi Rais ana imani nao na ana uhakika kuwa wanaweza kushirikiana naye kufanyakazi kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Hivyo na sisi tunaamini kwamba, hatua ya Rais kuendelea nao akiwabakiza kwenye nafasi zao za awali na kuongeza wengine wapya kutoka kwenye maeneo mengine wakiwamo wapinzani ni jitihada za kutaka umoja, uchapakazi na uwajibikaji zaidi, hivyo wateule hao wasimwangushe kiongozi aliyewapa dhamana hiyo. Kutokana na hilo, tunawakumbusha wateule wote kuwa baada ya kula kiapo, waende wakachape kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma na siyo kuendeleza ubabe na kujifanya miungu watu na kutisha raia na wafanyabiashara.

Ikumbukwe kuwa, katika moja ya ahadi zake, Rais aliwahi kusema, atateua watu bila kujali vyama wanavyotoka, bali atazingatia weledi na uadilifu, hivyo inawezekana nyie mlioteuliwa ni wale ambao mmekidhi vigezo alivyotaja hasa uadilifu na utumishi unaojali watu na siyo maslahi binafsi.

Mkumbuke kuwa siyo kwamba ninyi ni mabingwa, bali wapo wengi waadilifu na kwamba kuna Watanzania maelfu kwa mamia waadilifu, wacha Mungu na wachapakazi, lakini haiwezekani wote wakawa wakuu wa mikoa, hivyo msijisahau.

Baadhi ya viongozi kwenye uteuzi huo, huenda wana upungufu, lakini siyo wakati wa kuchambua kasoro bali kila anayepewa mkoa au taasisi kuiongoza aanze kujifunza na kuzingatia sifa za kiongozi bora ikiwamo uadilifu, hofu ya Mungu, kuthamini watu, kuheshimu kazi yake, kuachana na ubadhirifu na matumizi mabaya ya ofisi pamoja na kuendekeza mazoea ya kujinufaisha, ufisadi na rushwa.


Tunategemea viongozi wapya watakaokuwa wawazi, majasiri, wenye subira, wanaofanyakazi kwa uwajibikaji na ubunifu ambazo pia ni sifa nyingine za kumfanya mtu kuwa kiongozi bora zama hizi za uongozi wa kiujasiriamali.

Kikubwa zaidi ni kwamba, uongozi ni dhamana ya muda ambayo mtu anapoipata, anapaswa kuitendea haki huku ukijua kuwa kuna wakati hutakuwa na nafasi hiyo tena na kufahamu kuwa kuna maisha baada ya ukuu wa taasisi unayoiongoza. Kama ambavyo Rais amewateua kuwa viongozi bila kujali vyama vyenu, ni muhimu kila mmoja kufanya kazi kwa kushirikiana na watu wote bila ubaguzi wa kivyama, itikadi, kanda, jinsia, dini wala kabila kwa sababu maendeleo hayana dini wala kabila ili kutumiza malengo ambayo serikali imejiwekea kwa ajili ya Watanzania.

Licha ya kuwapo na mambo mema na upungufu kwa kila binadamu viongozi wakumbuke kuwa moja ya kauli za Rais Samia kwa watendaji ni kile alichosema hatarajii kuona viongozi aliowateua kuwaongoza wananchi wananyanyua mabega na zaidi wanafanya mambo ambayo yanawavuruga wananchi ambao wakati mwingine wanalazimika kubeba mabango kutoa kero zao. Kwa hiyo pamoja na kuwatakia kila la heri kwenye kazi zenu tunawakumbusha kuepuke ubinafsi, kujitukuza, kukandamiza watu na wakati mwingine kutumia jina la Ikulu kwa manufaa binafsi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wazazi wafuatilie mienendo ya wanafunzi, kuzurura vituoni

**WANAFUNZI** wanaoishi kwenye majiji, mijini na hata kwenye miji midogo ambao wanahitaji kutumia usafiri wa umma ili kufika shuleni au kurudi nyumbani, wanakumbana na kero nyingi hasa za usafiri zinazowachelewesha kufika shuleni na kurudi nyumbani kwa wakati.

Hali hiyo inatokana na tabia ya baadhi ya makondakta na madereva wa mabasi kama daladala, kuwazuia wasipande magari yao kwa madai kuwa nauli yao ni ndogo na wakati mwingine hulazimishwa kutoa nauli ya mtu mzima ili wapate usafiri na hata kuruhusiwa kukaa kwenye viti kwa haraka.

Kutokana na usumbufu wa usafiri kwenye daladala, baadhi ya wanafunzi wanakumbana na shida nyingi, zinazochangia wachelewe vipindi darasani, kwa kuwa hawafiki kwa wakati. Lakini kwa upande mwingine wapo pia makondakta na madereva wema ambao huwaruhusu wanafunzi kuingia kwenye mabasi kwa idadi fulani kulingana na nafasi, kwa kuwa wanatambua umuhimu wa elimu na ugumu wa usafiri.

Wapo baadhi ya watu vituoni wanaojitolea kuwahudumia wanafunzi kwa kuwapanga kwenye mistari na kusimamia foleni yao hadi wanapofika na kuingia kwenye magari. Hilo linatokea kwenye foleni za mabasi Mbezi Dar es Salaam.

Kama jamii ni jukumu la kila mmoja kusaidia wanafunzi kufika shuleni kwani ni muhimu watoto wakawahi masomo darasani hata hivyo, pamoja na hayo, wapo baadhi ya wanafunzi ambao iwe ni asubuhi au jioni, hufika katika vituo vya daladala na kukaa kwenye magenge na kuanza 'kupiga soga', bila kujali kwamba wanatakiwa kuwahi shuleni au nyumbani.

Kondakta anaweza kuwaita wapande gari wawahi shuleni au nyumbani, lakini hutoa majibu ya kejeli kana kwamba, wana usafiri wao na kumbe ndiyo huo huo wa daladala wanaoutegemea.

Wanafunzi wenye mtindo huo ni wale wanaovaa sare za shule na hasa suruali kwa mtindo wa mlegezo na tena wakining'iniza vitambaa kwenye mifuko ya nyuma ya suruali zao.

Pengine wakati umefika sasa wanafunzi wanaozurura vituo vya daladala wamulikwe na kuchukuliwa hatua ili waachane na tabio hiyo ambayo haina manufaa kwa maendeleo yao kielimu. Si vibaya kila mzazi na mlezi akafuatilia mwenendo wa mtoto anapokwenda shule na hata anaporudi, kwa kuwa inashangaza kukuta wanafunzi katika vituo vya daladala saa 12 jioni wakijifurahisha vituoni kwa 'kupiga soga'.

Vilevile inashangaza kuona wanafunzi wakiwa kwenye vituoni saa mbili au saa tatu asubuhi wakiendelea na michapo wakati wakijua kuwa huo ni muda wa masomo.

Japo baadhi ya makondakta na madereva wa daladala ni wakorofi, lakini wanafunzi wanaoshinda katika vituo vya daladala bila sababu za msingi, wasitumie mwanya huo kuwasukumia lawama.

Wanafunzi wanaijua umuhimu wa shule, hawawezi kutoka nyumbani na kwenda kukaa kwenye vituo vya daladala na kuanza kupiga soga, badala yake watatafuta usafiri kuwahi shule. Sambamba na hilo, wanafunzi wanaojua umuhimu wa elimu, wakitoka shule, watatafuta usafiri haraka ili kuwahi nyumbani upata muda wa kutosha wa kujisomea, siyo kuzurura kwenye vituo vya daladala.

Katika mazingira hayo, wapo baadhi ya wanafunzi ambao wakati mwingine, hulazimika kutembea umbali mrefu kuwahi shule au nyumbani pale wanapokosa usafiri wa daladala kwa wakati.

Wakati ukorofi wa makondakta na madereva wa daladala kwa wanafunzi ukijulikana, vilevile ingefaa kuufuatilia ukorofi wa baadhi ya wanafunzi ili hatua za kuwaondoa kwenye mazoea hayo hatari, zichukuliwe haraka.

Mzazi au mlezi anaweza kudhani kuwa mtoto yuko shule anaendelea na masomo na kumbe anasogoa kwenye vituo vya daladala, na pia anaweza kudhani kuwa anatakaliwa kupanda daladala lakini sivyo, hivyo aanze kufuatilia asiishi mazoea.

HABARI KITAIFA

# Wabunge wateule CCM waahidi ushirikiano Kigoma

**Na Deogratius Nsokolo,** KIBONDO

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema kitasimamia ahadi zote zilizotolewa na wabunge wateule kupitia chama hicho, Dk. Florence Samizi katika Jimbo la Muhambwe na Eliadory Kavejuru, Jimbo la Buhigwe.

CCM iliibuka na ushindi katika uchaguzi mdogo wa ubunge katika majimbo ya Muhambwe wilayani Kibondo na Buhigwe wilayani Buhigwe, katika uchaguzi uliofanyika jumapili.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara, Christine Mndeme, alisema baada ya kutangazwa kwa matokeo na wagombea wa chama hicho kuibuka washindi, kunaonyesha jinsi wananchi walivyo na imani na chama tawala na ilani yake ya uchaguzi.

Alisema wagombea waliahidi ahadi mbalimbali katika majimbo yao na kuwaondoa wasiwasi wananchi kuwa chama kitasimamia utekelezaji wake kupitia kwa wabunge wao.

Katika Jimbo la Muhambwe Msimamizi wa uchaguzi Diocles Lutema, alimtangaza Dk. Samizi kuwa mshindi kwa kupata kura 23, 441 na kumshinda mgombea wa ACT-Wazalendo Julius Masabo aliyepata kura 19,847 na Philip Fumbo wa Democratic Party (DP), aliyepata kura 368.

Katika Jimbo la Buhigwe, Msimamizi wa Uchaguzi, Marrycelina Mbehoma, alimtangaza Eliadory Kavejuru kuwa mbunge mteule wa jimbo hilo baada ya kupata kura 25,274 na kuwashinda wagombea wenzake 12.

Uchaguzi katika Jimbo la Muhambwe umefanyika baada ya aliyekuwa Mbunge wa jimbo hilo, Atashast Nditiye, kufariki dunia kwa ajali na katika Jimbo la Buhigwe uchaguzi umefanyika baada ya aliyekuwa Mbunge wa jimbo hilo, Dk. Philip Mpango kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Akitoa shukrani kwa wapigakura, Mbunge mteule wa Jimbo la Muhambwe Dk. Samizi, ameahidi kushirikiana na watu wote kuleta maendeleo katika jimbo hilo.

Alisema bado Kibondo ina tatizo la maji, elimu, afya, miundombinu na kilimo, linalohitaji ushirikiano kutatua.

Naye Kavejuru Mbunge mteule wa Jimbo la Buhigwe, alisema azma yake ni kuona jamii inakuwa na maisha bora kutokana na rasilimali mbalimbali zinazopatikana katika wilaya hiyo.

## Makandarasi wadai zaidi ya bil. 800/-

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

MADENI ya makandarasi na wahandisi washauri wanaoidai serikali yanazidi kuongezeka na kufikia Sh. bilioni 869.026.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Leonard Chamuriho, aliliambia Bunge kuwa deni hilo ni hadi kufikia Aprili, mwaka huu na changamoto kubwa ni upungufu wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo.

Alisema mkakati uliowekwa na serikali kukabiliana na hali hiyo ni kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha fedha za miradi zinalipwa kwa wakati, ili kupunguza gharama za riba inayoendelea kuongezeka.

Kadhalika, kuchelewa kutolewa kwa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT), jambo lililosababisha utekelezaji wa miradi ya barabara, madaraja, viwanja vya ndege na vivuko kuchelewa kuanza.

Alisema mkakati uliowekwa na wizara hiyo ni kuunda kitengo cha wataalamu wenye weledi na ujuzi wa kupitia nyaraka kwa kina na kuwasilisha Wizara ya Fedha kwa hatua za haraka.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Moshi Kakoso, alisema ucheleweshwaji wa malipo kwa makandarasi na wahandisi washauri kuna athari katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kiasi kikubwa.

Alisema athari mojawapo ni baadhi ya miradi kusimama au kutekelezwa kwa kasi ndogo pamoja na kuongezeka kwa riba.

Alisema hadi Februari, mwaka huu, zimetolewa Sh. bilioni 301.023 za Mfuko wa Barabara zilizotumika kulipa makandarasi wa ndani wanaofanya kazi za matengenezo na ukarabati wa barabara.

Kwa mujibu wa Kakoso, kiasi cha fedha kilichotengwa kwa miradi ya maendeleo na kiasi kilichotolewa hadi Februari mwaka huu ni kidogo jambo lilioathiri utekelezaji.

Alisema kiasi kilichokuwa kimetengwa ni zaidi ya Sh. trilioni 1.5 na kilichotolewa ni zaidi ya Sh. bilioni 772 sawa na asilimia 49.

Pia alisema kuna changamoto ya makandarasi wa ndani kuwa na uwezo mdogo wa mtaji na kushindwa kushiriki kikamilifu katika fursa za kazi kutokana na masharti ya upatikanaji wa dhamana za zabuni.







**CHAMA CHA WAFANYAKAZI MASHAMBANI NA KILIMO TANZANIA**

**TANZANIA PLANTATION AND AGRICULTURAL WORKERS UNION**
**(TPAWU)**
**S.L.P 77420, DAR ES SALAAM, SIMU 2182496,**
**Barua pepe: tpawuheadquarter@yahoo.com**

**TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA UCHAGUZI**
**TAREHE 25 AGOSTI, 2021**

Mkutano Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi Mashambani na Kilimo Tanzania (TPAWU) utafanyika tarehe 25 Agosti 2021, Mkoani Dodoma.

Tangazo hili linatolewa kwa mujibu wa ibara ya 9.1 na 9.6 ya Katiba ya TPAWU toleo la 6 la mwaka 2013, Katiba yenye mamlaka kutokana na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini namba 6 ya mwaka 2004 kifungu cha 47.

Agenda za Mkutano Mkuu wa chama ni:-
1. Kufungua mkutano.
2. Kuthibitisha akidi na agenda za mkutano.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa mkutano mkuu uliopita.
4. Uchaguzi Mkuu wa viongozi na watendaji ngazi ya taifa.
5. Kufunga mkutano.

Kwa mujibu wa katiba ya TPAWU toleo la mwaka 2013 kifungu 9.9.2 Mkutano Mkuu wa Chama utachagua viongozi wafuatao:-

i. Mwenyekiti wa Chama wa Taifa
ii. Katibu Mkuu wa Chama wa Taifa
iii. (a) Wajumbe 8 wa Baraza Kuu TPAWU, mmoja kutoka kila Kanda
(b) Wajumbe 8 wa Baraza Kuu la TUCTA
(c) Wajumbe 16 wa Mkutano Mkuu TUCTA kwa kufuata katiba ya Shirikisho.
iv. Mjumbe mmoja mwakilishi wa wanawake kwenye mkutano wa Shirikisho.
- Kwa utaratibu hapo juu, nafasi yenye wajumbe zaidi ya mmoja jinsia izingatiwe.

v. Kamati ya wanawake Taifa kifungu 5.4.1

Mkutano Mkuu wa Wanawake utachagua wafuatao:-
(a) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa
(b) Wajumbe 4 watakaohudhuria Baraza Kuu
- Wajumbe wake ni wanawake wote wa Mkutano Mkuu.

vi. Kamati ya Vijana Taifa – kifungu 6.1.3
Wajumbe watachagua wafuatao:-
(a) Mwenyekiti wa Vijana Taifa
- Wajumbe wake ni vijana wote waliopo katika Mkutano Mkuu.

vii. Baraza Kuu kwa mujibu wa kifungu 10.2.1 (v, vi, ix na x) Baraza Kuu litachagua viongozi wafuatao:-
(a) Naibu Katibu Mkuu
(b) Wajumbe 3 wa Kamati ya Utendaji (jinsia izingatiwe)
(c) Mjumbe 1 Kamati ya Utendaji TUCTA

**MUDA WA KUCHUKUA NA KURUDISHA FOMU**
Kwa mujibu wa kifungu 9.1. cha Katiba ya TPAWU, "Kabla ya uchaguzi wa viongozi Kitaifa Katibu Mkuu atatangaza nafasi zote za uongozi katika chama kuwa ziko wazi, wanachama wenye sifa watakaopenda kugombea nafasi hizo watajaza fomu na kuzirejesha ofisi ya Katibu Mkuu ndani ya kipindi kitakachoainishwa katika tangazo" na kifungu 9.6 cha Katiba ya TPAWU, "Taarifa ya Mkutano Mkuu wa chama itatolewa miezi mitatu kabla ya Mkutano Mkuu wa uchaguzi. Taarifa ya muda mfupi inaweza kutolewa kama itabidi kuitisha Mkutano Mkuu maalum".

Fomu za uongozi ngazi ya Taifa zitaanza kutolewa tarehe 15 June 2021 na mwisho wa kurejesha fomu hizo ni tarehe 15 Agosti, 2021, na zitatolewa na kurejeshwa kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika siku za kazi Jumatatu hadi Ijumaa.

Waombaji wa nafasi za uongozi wazingatie kuwa fomu zitakazorejeshwa baada ya tarehe ya mwisho au muda wa mwisho uliotajwa katika tangazo hili hazitapokelewa. Pia izingatiwe kuwa fomu ambazo hazikujazwa na kukamilika hazitapokelewa.

WANACHAMA MNAHAMASISHWA KUSHIRIKI KIKAMILIFU ILI KUPATA VIONGOZI BORA WA KULINDA NA KUTETEA MASLAHI YA WAFANYAKAZI "MSHIKAMANO DAIMA"

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA TAREHE 18/5/2021**
**KABENGWE NDEBILE KABENGWE**
**KATIBU MKUU - TPAWU**

# Samia: Majaji katendeni haki

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana amewaapisha majaji wa Mahakama Kuu na wa Mahakama Rufani 28 huku akiwaagiza kwenda kutenda haki.

Rais Samia aliwaonya majaji hao kwa kuwaeleza kuwa atakayekwenda kinyume na maadili ya kazi, akibainika kushindwa kutenda haki atakuwa amekosa sifa ya kuendelea na kazi.

Uapisho wa majaji hao saba wa Mahakama ya Rufani na 21 wa Mahakama Kuu ulifanyika jana, Ikulu ya Dar es Salaam.

"Wito kwa majaji wote ni kwamba, jukumu lililo mbele yenu ni kubwa sana. Dhima ya utoaji haki inabebwa na ninyi. Haki ni msingi wa maendeleo, penye haki kuna amani, kuna maelewano na pia shughuli za kisiasa na kijamii zina nawili kunapokuwa na haki, hivyo mkatekeleze majukumu yenu kwa uadilifu mkubwa, naomba kiapo kile muende nacho."

"Nawaombeni mkaongoze na kuongozwa vyema na nafsi zenu. Katika utendaji wa haki, kanuni na sheria zinazotungwa na bunge, asilimia 70 ni ya kazi yenu, lakini asilimia 30 mkaongozwe na utu na imani zenu na nafsi zenu."

Alisema kama nafsi inaelekeza kwenda kuchukua fedha na kunyima haki ya mwingine na kumpa mwingine ni kuwa umeshatetereka na ukikugundulika utakuwa umeshakosa sifa zilizokupandisha kufika hapo.

Rais Samia alisema katika uteuzi wa majaji hao, alizingatia usawa wa kijinsia na alifanya hivyo kwa kuzingatia vigezo na sifa walizonazo.

"Kati ya majaji saba wa Mahakama ya Rufani, watatu ni wanawake na kati ya 21 wa Mahakama Kuu, karibu 10 kati ya hao ni wanawake. Hii inaonyesha dhahiri kauli niliyoisema ya kuongeza wanawake katika nafasi za uongozi, nimezingatia uwezo na si uanawake tu. Ombi langu kwenu mkajiamini na kufanya kazi kama inavyotakiwa," alisema Rais Samia.

Kwa upande wake Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahimu Juma, alisema idadi ya majaji wa Mahakama wa Rufani imeongezeka kutoka 17 hadi 21 huku wa Mahakama Kuu imeongezeka hadi kufikia 86.

Profesa Juma alisema kabla ya kuapishwa kwa majaji hao saba wa Mahakama ya Rufani, majaji waliokuwapo walikuwa wanasikiliza mashauri kwa kuunda majopo matano kwa majaji watatu watatu, kwamba uwezo wa kuamua na kusikiliza rufani kwa jopo moja ilikuwa ni mashauri 28 hadi 36 katika kikao kimoja.

Alisema kwa sasa baada ya kuongezeka kwa majaji hao watakuwa na uwezo wa kusikiliza na kumaliza mashauri kwa haraka na kupunguza mzigo mkubwa uliokuwapo na kupunguza pia mrundikano wa mashauri mahakamani.



Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Pwani, Alban Kihulla, akifafanua jambo kwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, alipotembelea kituo cha Misugusugu jana. Kulia ni Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stella Kahwa. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Mwambe aonya watumishi waomba rushwa wawekezaji

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe, amewaonya watumishi wa wizara yake kuwa mtu yeyote atakayeomba rushwa kwa mwekezaji ataonyeshwa mlango wa kutokea haraka.

Aliyasema hayo jana wakati akiwa na Naibu wake, William Ole Nasha, walipotembelea Kituo cha Uwekezaji (TIC) na kuzungumza na wafanyazi na viongozi wa kituo hicho.

Waziri Mwambe alisema huduma za serikali haziuzwi wala kutolewa kwa misingi ya rushwa na kwamba mtumishi yeyote atakayethubutu kuomba na kupokea rushwa ajue anahatarisha ajira yake.

Pia, aliwaonya baadhi ya wawekezaji wanaowashawishi watumishi wa TIC kupokea rushwa kuwa alipokuwa Mkurugenzi wa kituo hicho aliwashughulikia kwa kutaifisha fedha walizotoa kama hongo.

Alitoa wito kwa viongozi wa TIC kushirikiana na Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), kuwa na mijadala kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu uwekezaji na wafanyabiashara.

Alionya pia tabia ya baadhi ya viongozi kuwalipisha faini na adhabu mbalimbali wawekezaji bila kuzungumzia nao kujua shida zao kwa kuwa hali hiyo inawatisha wawekezaji wapya.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan, amewapa jukumu la kurejesha imani kwa wawekezaji na wanapaswa kuweka mazingira ambayo yatawavutia kuja kuwekeza kwa kuondoa vikwazo. Pia aliagiza viongozi wa TIC kuhakikisha wanazifungua upya ofisi za kituo hicho zilizoko mikoani ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wawekezaji.

Alisema ili Watanzania wajue zaidi kuhusu shughuli za kituo hicho, lazima kuwe na vipindi vya elimu kwa umma kwenye vyombo mbalimbali vya habari kuhusu uwekezaji.

# Kilio cha wabunge ujenzi barabara chatawala bungeni

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

KILIO cha uhaba wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara jana kilitawala bungeni, huku mmoja akiomba ridhaa ya Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, apige sarakasi hadi kwenye meza ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kuonyesha uzito wa kilio cha wananchi.

Wabunge hao walisema kuna barabara ziliahidiwa na marais wanne, lakini hadi leo hakuna kilichofanyika huku wengine wakipewa fedha za ukarabati, na kupendekeza kujengwa kwa kilomita chache ambazo zitakamilika kuliko kuwa na nyingi.

Kilio hicho walikitoa wakati wakichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wiraza ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka 2021/22, ambayo iliomba zaidi ya Sh. trilioni 3.747.

Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini (CCM), Flatey Massay, aliyeomba ridhaa ya kuruka sarakasi ndani ya Bunge, alisema barabara ya Karatu, Mbulu, Hydom na Sabiti yenye urefu wa kilomita 389 ni ahadi ya marais wanne, lakini hadi sasa haijaanza kujengwa.

"Nimeshauliza maswali 20 na michango mitano ndani ya bunge hili, mara ya kwanza niliambiwa iko kwenye upembuzi yakinifu, ya pili yakinifu, ya tatu mipango na usanifu na michoro, hii barabara iko kwenye ilani ya chama, lakini bado imesahaulika," alisema na kuongeza;

"Mwaka jana walisema watajenga kilomita 50 sasa wanasema kilomita 25. Mheshimiwa Naibu Spika naomba uniruhusu niruke sarakasi, niruke! Niruke! Hadi pale alipo waziri ili nifikishe kilio cha wananchi wa Mbulu. Naomba mgawe rasilimali kwa usawa," alisema.

Aidha, alisema mawaziri watatu tofauti walitoa ahadi za kujenga na wakiondoka hakuna kinachoendelea.

Mbunge wa Iramba Mashariki (CCM), Francis Mtinga, alisema wakati wabunge wengine wanaomba fedha za ukarabati wengine hawana hata kilomita moja ya lami, kiasi cha kujiuliza wanaishi nchi gani.

Mbunge wa Jimbo la Bukene (CCM), Suleiman Zed, alisema kila mwaka kuna orodha ndefu ya barabara zitakazojengwa lakini utekelezaji hauzidi robo ya kilichotarajiwa.

"Kuliko tuseme tutajenga barabara 200, bora tuseme zitajengwa 50. Pia tufanye marekebisho ya sheria ya fedha ili zitolewe zote kwa wakati mmoja. Mfano bajeti iliyopita zilitengwa Sh. trilioni 1.5 zilitolewa Sh. bilioni 900 na Sh. bilioni 600 hazikutoka," alisema.

Mbunge wa Jimbo la Kyela, Ally Mlaghila, alisema ni muhimu kufuatilia kwa karibu ujenzi wa barabara kwa kuwa nyingi zinaharibika baada ya muda mfupi huku akitoa mfano wa barabara ya Dodoma hadi Iringa ambayo sasa inakarabatiwa.

Pia barabara ya Uyole Kasumulo, ambayo ilijengwa miaka 30 iliyopita na ina ubora mpaka sasa, huku ya Dodoma Iringa haina miaka 10 imeshaanza kukarabatiwa.

Kutokana na hoja hiyo, Naibu Spika Dk. Ackson alisema ni muhimu sana kufuatilia kwa karibu kwa kuwa inashangaza barabara kubomoka haraka licha ya kutumia fedha nyingi.

Aliwashauri wabunge wanapotembelewa na mawaziri kwenye majimbo yao kuwapitisha barabara korofi ili waone hali halisi, huku akitoa mfano wa yeye kusota barabarani hadi usiku akitoka Kigoma kwenda Mbeya.

## HABARI KITAIFA

# Simbachawene abaini dosari Uhamiaji Mwanza

**Na Richard Makore,** MWANZA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, amesema baadhi ya maofisa wa Idara ya Uhamiaji mkoani Mwanza wanaendesha operesheni ya kuwabaini wahamiaji haramu kwa maslahi binafsi.

Amesema maofisa hao wanaendesha msako wa kuwakamata wahamiaji haramu pasipo uongozi kujua. Kutokana na hali hiyo, aliahidi kumkabidhi Ofisa Uhamiaji wa Mkoa wa Mwanza, Bahati Mwaifuge, majina ya maofisa hao.

Waziri Simbachawene aliyaeleza hayo wakati akizungumza na viongozi wa uhamiaji mkoani Mwanza.

Alisema msako wowote wa wahamiaji ama watu wasiokuwa raia ni lazima ufuate utaratibu na siyo watumishi kuamua kuingia mtaani na kufanya kazi hiyo kwa maslahi yao binafsi.

"Nina majina ya watu hao kama unataka nitakukabidhi, usifikiri sifahamu mchezo huo kwa watumishi walio chini yako," alisema Simbachawene.

Alisema ni lazima kila kitu kinachofanyika na mtumishi ama ofisa wa Uhamiaji kijulikane badala ya watu wachache kuamua kuanzisha msako wa bila ofisi kufahamu.

Simbachawene aliitaka idara hiyo kuongeza mkazo katika kudhibiti wahamiaji haramu.

Alisema wahamiaji haramu wanawanyima fursa Watanzania na lazima idara hiyo iongeze nguvu husus ani maeneo ya mipakani.

Ofisa Uhamiaji mkoani Mwanza, Bahati Mwaifuge, alimweleza Waziri Simbachawene kuwa wamefanikiwa kumkamata kinara wa aliyekuwa akiingiza wahamiaji haramu hapa nchini.

Bahati alisema tangu walipomkamata kinara huyo tatizo hilo limepungua, na sasa ofisi yake imeanza kutoa hati ndogo za kusafiria kwa ngazi za wilaya, huku ofisi ya mkoa ikitoa hati kubwa za kusafiria.

Waziri Simbachawene pia alitembelea Jeshi la Polisi mkoani Mwanza na kukutana na mahabusu waliowekwa rumande katika kituo kikuu cha polisi.

Maeneo mengine aliyotembelea ni pamoja na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

# SUMAJKT yanunua vitendea kazi vya bil. 2.9/-

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT), limejiimarisha kiutendaji na kiulinzi kwa kununua magari 180, pikipiki 102, mitambo 52 na mashine sita, vyote vikiwa na thamani ya Sh. bilioni 2.9.

Naibu Mkurugenzi wa SUMAJKT anayeshughulikia masuala ya Operesheni, Kanali Erasmus Bwegoge, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akiikabidhi Kampuni ya SUMAJKT Guard magari sita mapya yaliyonunuliwa kwa thamani ya Sh. milioni 385.8.

Alisema magari hayo yamekuwa yakinunuliwa kila mara kwa lengo la kuongeza mapato ya kampuni kwa sababu kutokana na miradi mingi ililazimika kuyakodi kwa watu wengine. Alisema ununuzi wa vitendea kazi hivyo utaondoa matatizo hayo na kuokoa kiasi cha fedha ambacho kingetumika kukodi.

Alisema kati ya magari 180, magari 31 yalinunuliwa katika kipindi cha kuanzia Oktoba, 2019 hadi Mei, mwaka huu.

Alisema mashine na mitambo sita na pikipiki 12 zilinunuliwa katika kipindi tajwa hapo juu. Aliwataka watakaokabidhiwa magari hayo mpya wahakikishe wanayatunza ili yalete tija kwa JKT na taifa.

Mkurugenzi Mwendeshaji SUMAGUARD, Luteni Kanali, Joseph Masanja, alisema ununuzi wa magari hayo umefanya kampuni iwe na jumla ya magari 39 ambayo yanatumika katika operesheni na utawala.

# M/kiti Serikali ya Mtaa adaiwa kuua na kukimbia

**Na Richard Makore,** MWANZA

MWENYEKITI wa Serikali ya Mtaa wa Nyambiti, Kata ya Buzuruga, wilayani Ilemela jijini Mwanza, Itare Zeba, amekimbia nyumbani kwake na kwenda kujificha kusikojulikana baada ya kudaiwa kumuua mkazi wa mtaa wa Miti Mirefu, Denis Petro (20), aliyemkamata na kumweka ofisini kwake.

Hii ni mara ya pili kwa mwenyekiti wa serikali ya mtaa kudaiwa kufanya mauaji, mara ya kwanza mwenyekiti wa serikali ya mtaa wa Kishiri jijini Mwanza, alidaiwa kumuua kijana mmoja aliyemtuhumu kuwa kibaka.

Mwenyekiti huyo anadaiwa kumkamata Petro akiwa na wenzake kwa madai ya kutembea usiku katika mkesha wa sikukuu ya Eid.

Ilidaiwa kuwa siku aliyokamatwa alikuwa na wenzake wawili akitokea nyumbani kwa bibi yake anayeishi mtaa wa Nyambiti.

Akisimulia mkasa huo mama wa marehemu, Lucy Aron, alisema siku ya Ijumaa alikula chakula na mtoto wake na siku iliyofuata alipata taarifa kwamba mtoto wake alikamatwa usiku.

Alisema baada ya kupata taarifa hiyo, alianza kuwasiliana na ndugu zake ili wakamtoe huko alipopelekwa.

Alisema alipata taarifa kwamba mtoto wake amefariki baada ya kudaiwa kupigwa na kupelekwa ofisi ya serikali ya mtaa wa Nyambiti.

Aliongeza kuwa vijana wengi wanapigwa na kukandamizwa huku akiomba haki itendeke.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne Muliro, akizungumzia sakata hilo, alisema hajapata taarifa hizo na kwamba akipata undani wake atalifanyia kazi suala hilo.

Aliwataka ndugu wa marehemu kutoa taarifa kituo cha polisi kama wana malalamiko ili wafuatilie.

Hata hivyo, alisema wenyeviti wengi wa serikali za mitaa hawapendwi na watu wanaotenda maovu kwa jamii na tukio hilo halijatolewa taarifa katika kituo chochote cha polisi.

Akizungumzia matukio ya watu kujichukulia sheria mkononi, akiwa jijini Mwanza jana, Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, alikemea vitendo hivyo na kutaka sheria ifuatwe.


## NOTISI/ TANGAZO

**REAL MASTER COMPANY LTD,NUTMEG AUCTIONEERS AND PROPRTY MANAGERS CO.LTD,MASHOKA AUCTION MART,BEST GROUP,WAUNGWANA AUCTION MART,MASETO AUCTIONEERS AND DEBT COLLECTORS LTD,TAUSI AUCTION MART AND CHAMPION AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| NA | JINA LA MDAWA | TAWI ALILOKOPA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ARSEN LEONARD SHIRIMA | ARUSHA | ARSEN LEONARD SHIRIMA | NYUMBA | KATA YA DARAJA MBILI MTAA WA KATI | 3/06/2021 NA KUENDELEA |
| 2 | ZEPHANIA PAUL MASANGU | MWANZA | ZEPHANIA PAUL MASANGU | BOMA | NYASAKA CENTRE-MWANZA | 03/06/2021 NA KUENDELEA |
| 3 | FASILI WILLIAM RITTE | MWANZA | FASILI WILLIAM RITTE | NYUMBA | BUJINGWA-BUSWELU | 04/06/2021 NA KUENDELEA |
| 4 | SIKITU HAMIS YAHAYA | MWANZA | HAJI ABEID KASUBI | NYUMBA | NYASAKA'A' – MWANZA | 05/06/2021 NA KUENDELEA |
| 5 | VICENT MICHAEL KILEO | MOSHI | VICENT MICHAEL KILEO | NYUMBA | KINDI -KIBOSHO KILIMANJARO | 03/06/2021 NA KUENDELEA |
| 6 | SABAS PAUL MSELE | MOSHI | SABAS PAUL MSELE | NYUMBA YENYE HATI | SHIRIMATUNDA MOSHI KILIMANJARO - | 04/06/2021 NA KUENDELEA |
| 7 | DANIEL ELISAMIA KIMARO | MOSHI | DANIEL ELISAMIA KIMARO | NYUMBA | SHABAHA MABOGINI MOSHI KILIMANJARO - | 04/06/2021 NAKUENDELEA |
| 8 | MIRIAM BALTAZAR TEMU | MOSHI | MIRIAM BALTAZAR TEMU | NYUMBA | BOMANGOMBE LINE POLICE HAI KILIMANJARO | 05/06/2021 NA KUENDELEA |
| 9 | ANTHONY JOHN MUSHI | MOSHI | ANTHONY JOHN MUSHI | NYUMBA | TAWINGO-URU MOSHI | 05/06/2021 NA KUENDELEA |
| 10 | MWIDINI SADIKI RAJABU | MOSHI | MWIDINI SADIKI RAJABU | NYUMBA | MERALI SANYA JUU SIHA | 12/06/2021 NA KUENDELEA |
| 11 | WITNESS STIVINI MMARY | MOSHI | WITNESS STIVINI MMARY | NYUMBA | NGARENAIROBI -SIHA | 12/06/2021 NA KUENDELEA |
| 12 | ALLEN BARAKAEL MMARI | MOSHI | ALLEN BARAKAEL MMARI | NYUMBA | FUKA-SIHA-SANYA JUU | 18/06/2021 NA KUENDELEA |
| 13 | SENORA SHABANI MDEE | MOSHI | SENORA SHABANI MDEE | NYUMBA | YAMU MAKAA KAWAWA MOSHI | 24/06/2021 NA KUENDELEA |
| 14 | PRISCUS ERNEST TARIMO | MOSHI | SANGIWA YAHAYA MSANGI | NYUMBA | MABOGINI JUU MOSHI KILIMANJARO | 24/06/2021 NA KUENDELEA |
| 15 | SALIM DAUDI NGOWI | MOSHI | ATHUMANI PETRO MWIRE | NYUMBA | TELA KUSINI UCHIRA MOSHI KILIMANJARO | 24/06/2021 NA KUENDELEA |
| 16 | PETER WILFRED ISANGYA | MOSHI | PETER WILFRED ISANGYA | NYUMBA | KARANSI SIHA-SANYA JUU KILIMANJARO | 03/07/2021 NAKUENDELEA |
| 17 | KANAEL SIMON NNKO | MOSHI | KANAEL SIMON NNKO | NYUMBA | UWIRO USA RIVER ARUSHA ARUMERU | 03/07/2021 NA KUENDELEA |
| 18 | ZAKAYO LAZARO MOLELI | MOSHI | ZAKAYO LAZARO MOLELI | NYUMBA | OKOLIN KIDIRE SIHA-KILIMANJARO | 10/07/2021 NA KUENDELEA |
| 19 | **ASNA SAID NJEMA** | UBUNGO | **ASNA SAID NJEMA** | NYUMBA | VIGAZWA **CHALINZE** | 03/06/2021 NA KUENDELEA |
| 20 | **DOTTO HARUNA MSUYA** | UBUNGO | **DOTO HARUNA MSUYA** | NYUMBA | KIBAHA TANGINI. | 03/06/2021 NA KUENDELEA |
| 21 | **DORICA SIMON MEREMO** | UBUNGO | **DORICA SIMON MEREMO** | GARI AINA YA TOYOTA IST YENYE NAMBA **T293 DNS.** | MAKUMBUSHO | 05/06/2021 NA KUENDELEA |
| 22 | **ALPHONCINA R MBOYA** | UBUNGO | **ALPHONCINA R MBOYA** | NYUMBA | MBEZI MSAKUZI | 06/06/2021 NA KUENDELEA |
| 23 | **VERONICA CLEMENCE** | UBUNGO | **MARIAM HEROZON MBILINYI** | NYUMBA | BUZA KATA YA MAKANGARAWE. | 07/06/2021 NA KUENDELEA |
| 24 | **AMOS KHANGA PECHE** | TEGETA | **AMOS KHANGA PECHE** | NYUMBA | MBOPO MADALE | 08/06/2021 NA KUENDELEA |
| 25 | **ATHUMAN HASSAN HEMEDI** | TANDALE | **ATHUMAN HASSAN HEMEDI** | NYUMBA, | GONGOLAMBOTO | 05/06/2021 NA KUENDELEA |
| 26 | **SAMSON WAZAELLY MKUMBO** | KIJITONYAMA | **JUSTICE WILLIAM KATITI** | NYUMBA | MTAA WA NYAKASANGWE KATA YA WAZO | 08/06/2021 NA KUENDELEA |
| 27 | **VENANCE CLEMENCE** | TEGETA | **VENANCE CLEMENCE NYARI** | NYUMBA | WAZO | 08/06/2021 NA KUENDELEA |
| 28 | **FAUSTINE VICENT PETER** | KIJITONYAMA | **OKONYI OMARY ORAO** | NYUMBA | SALASALA KATA YA WAZO | 09/06/2021 NA KUENDELEA |
| 29 | **NEEMA ARON URIO** | KIJITONYAMA | **OMARI ATHUMANI MKINDI** | NYUMBA | MTAA WA KISIWANI KATA YA VIJIBWENI | 10/06/2021 NA KUENDELEA |
| 30 | **NICE CHANDE MOHAMED** | KIJITONYAMA | **ROSEMARY DESDELIUS** | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | MTONGANI WILAYA YA TEMEKE. | 07/06/2021 NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0754497396/ 0754 443904 / 0743885084/0715363537
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

# Ashauri ujenzi mabwawa kuhifadhi maji ya mvua

MBUNGE wa Bahi (CCM), Kenneth Nollo, ameitaka serikali kujenga mabwawa makubwa ambayo yatakayohifadhi maji ya mvua ili kutumika kwa shughuli za kibinadamu, kilimo na mifugo katika Mkoa wa Dodoma.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alisema mkoa huo umekuwa haupati mvua za kutosha.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, alijibu kuwa katika jitihada za kuboresha huduma ya maji kwa wananchi wa Dodoma, mwaka 2020/21, serikali imekamilisha usanifu kwa ajili ya kukarabati bwawa la Chikopelo lililopo umbali wa kilomita 70 kutoka Bahi mjini.

Alisema lengo ni kuongeza upatikanaji wa maji katika vijiji sita ukiwamo mji wa Bahi na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la Kidoka litakalohudumia vijiji saba ukiwamo mji wa Chemba.

"Ukarabati na ujenzi wa mabwawa hayo unatarajiwa kufanyika katika mwaka 2021/22 ikiwa ni pamoja na ujenzi wa malambo sita katika vijiji vya Mpamatwa, Uwelela, Kambia, Nyasa, Kolema Kuu, Kidoka na Palanga katika wilaya za Bahi na Chemba," alisema.

Vilevile, alisema serikali ina mpango wa kujenga bwawa la kimkakati katika Kata ya Farkwa na mpaka sasa usanifu umekamilika na ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaotakiwa kupisha eneo la mradi wa ujenzi wa bwawa hilo umefanyika kwa asilimia 99.

"Bwawa hilo lenye mita za ujazo milioni 470, linatarajiwa kujengwa kwa awamu kutegemea na upatikanaji wa fedha," alisema.

Alisema katika kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dodoma, serikali imechimba visima nane na kukarabati vitatu vya zamani.

"Kazi ya ufungaji wa miundombinu inaendelea na inatarajia kukamilika mwezi Juni 2021," alisema.




# Serikali kununua meli nne kukuza uchumi wa bluu

BUNGE limeelezwa kuwa kwa mwaka 2021/22, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimepanga kununua meli nne za uvuvi wa baharini ikiwa ni mkakati wa kukuza uchumi wa bluu.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fakharia Shomari Khamis.

Mbunge huyo alihoji wizara ina mpango gani wa kutoa elimu ya matumizi ya teknolojia kwa wavuvi wa bara na visiwani katika kukuza uchumi wa bluu.

"Serikali imesema ina mkakati wa kununua meli nane, je, meli hizo nane zitasaidiaje kutoa ajira kwa vijana," alihoji.

Akijibu swali hilo, Ulega alisema meli nane zimepangwa kununuliwa ambapo kati ya hizo nne ni za upande wa Zanzibar na zingine Tanzania Bara.

"Tukifanya hivyo mashirika yetu makubwa mawili ya ZAFICO (Shirika la Uvuvi Zanzibar) na TAFICO (Shirika la Uvuvi Tanzania), yanafufuliwa na yatanunua meli mbili kila upande kwa kuanzia mwaka 2021/22 na zitapatikana ajira kwa vijana wa kitanzania na watapewa elimu ya kujiandaa na fursa hiyo kubwa," alisema.

Pia alisema serikali imejipanga vyema kuhakikisha teknolojia ndio itakayoongoza katika kutumia rasilimali zilizopo kwenye bahari na maziwa makuu.

"Teknolojia hii ni pamoja na kuwasaidia wavuvi kutumia vifaa vya kisasa vitakavyowafikisha eneo walipo samaki kwa urahisi na kwa kutumia gharama nafuu, wizara inajipanga wavuvi watumie GPS ili anapoingia baharini awe na taarifa wapi samaki wanapatikana," alisema.

Pia alisema kuna mpango wa maendeleo ya kilimo awamu ya pili ambao utaenda sambamba na kuwaandaa vijana ikiwa ni pamoja shughuli nzima ya ufugaji wa samaki katika maeneo la bahari.

"Zaidi ya vijana 1,000 na wanawake 15,000 Zanzibar watanufaika na mradi huu, wananchi wajipange vyema kuhakikisha tunatumia fursa hii," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji serikali imejipanga vipi kupambana na tishio la uvuvi haramu nchini.

"Je, ni meli ngapi zilikamatwa nchini tokea mwaka 2015 - 2020 kwa kosa la uvuvi haramu," alihoji. Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ulega alisema ili kupambana na tishio la uvuvi haramu serikali imeandaa mkakati wa ulinzi na usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi.Alisema katika mpango huo ushirikishwaji wa jamii katika kusimamia na kulinda rasilimali za uvuvi kupitia Halmashauri, Serikali za Vijiji na vikundi vya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi (BMUs) utaimarishwa.

"Kupitia mkakati huo, serikali itaendelea kutoa elimu kuhusu athari za uvuvi haramu kwa mazingira, jamii na uchumi, pia, itafanya maboresho ya sheria ili kuwa na ya kisasa dhidi ya uvuvi haramu ikiwamo kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa kwa kushirikiana na nchi mbalimbali zikiwamo nchi za SADC katika kuzuia uvuvi haramu usioratibiwa na kuripotiwa," alisema.

Alisema katika Bahari Kuu, serikali imeimarisha na kuboresha mfumo wa ufuatiliaji wa mienendo ya meli za uvuvi VMS kutoka META Fisheries, uliotumika kuanzia mwaka (2010-2015), meli zilizofunga king'amuzi aina ya Argos pekee ndizo zilizoonekana.

"Kwa sasa serikali imeboresha mfumo wa TEHAMA katika usimamizi na ulinzi wa rasilimali za uvuvi kwa kuweka mfumo mpya wa 'Themis Web' ambao una uwezo wa kufuatilia mienendo ya meli zote za uvuvi bila kujali kama imefunga aina gani ya king'amuzi," alisema.

Kuhusu kukamatwa kwa meli ya uvuvi, Ulega alisema katika kipindi cha miaka mitano kuanzia (2015-2020) meli moja ya uvuvi haramu ilikamatwa Bahari Kuu na kufunguliwa mashtaka na mahakama iliamuru mmiliki wa meli hiyo kulipa jumla ya Shilingi bilioni moja au kufungwa jela miaka 20.



Mbunge wa Jimbo la Bahi, Keneth Nollo, akiuliza swali bungeni jana kwenye vikao vya Bunge la Bajeti vinavyoendelea jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wapiga ramli chonganishi, manabii wa uongo waonywa

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imesema katika kipindi cha mwaka 2020 wapiga ramli chonganishi 57 walikamatwa na kufikishwa mahakamani na kesi zao zipo katika hatua mbalimbali.

Hata hivyo, imewatahadharisha wananchi kujiepusha na waganga wapiga ramli chonganishi na manabii wa uongo kwa kuwa matendo yao husababisha hasara, mfarakano na vifo katika jamii.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Konde (ACT-Wazalendo), Khatib Said Haji.

Mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali kukabiliana na manabii na waganga matapeli.

"Serikali inachukua hatua gani kukabiliana na waganga wapiga ramli chonganishi na manabii wa uongo wanaodanganya na kuwatapeli wananchi kila siku," alihoji.

Naibu Waziri alijibu kuwa serikali kupitia Jeshi la Polisi ina jukumu la kulinda watu na mali zao na kuleta amani na utulivu miongoni mwa jamii ikiwa ni pamoja na kuzuia na kupambana na uhalifu wa aina yoyote usitokee.

"Katika kutekeleza majukumu hayo operesheni na misako ya mara kwa mara imekuwa ikifanyika katika kuwakamata waganga wapiga ramli chonganishi na manabii wa uongo wanaodanganya na kuwatapeli wananchi na kuwaletea hasara kubwa na mfarakano katika jamii kwa kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria," alisema.

Aliwataka wananchi kuendelea kujitokeza bila uoga kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi kuhusu vitendo hivyo viovu ili hatua stahiki zichukuliwe kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

## HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI, MHESHIMIWA MHANDISI DKT. LEONARD MADARAKA CHAMURIHO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22



Mhe. Mha. Dkt. Leonard M. Chamuriho (MB.)
**Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi**

Mhe. Mha. Godfrey M. Kasekenya (MB.)
**Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi**

Mhe. Mwita M. Waitara (MB.)
**Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi**

Mha. Joseph K. Malongo
**Katibu Mkuu wa Sekta ya Ujenzi**

Bw. Gabriel J. Migire
**Katibu Mkuu wa Sekta ya Uchukuzi**

# HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI, MHESHIMIWA MHANDISI DKT. LEONARD MADARAKA CHAMURIHO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia taarifa iliyowasilishwa humu Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2020/21 na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2021/22.

2. ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana leo kwa ajili ya kushiriki katika Mkutano wa Bunge lako ili kujadili utekelezaji wa majukumu ya Sekta za Ujenzi (Fungu 98) na Uchukuzi (Fungu 62) kwa mwaka wa fedha 2020/21 pamoja na kujadili Mipango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Sekta hizo kwa mwaka wa fedha 2021/22. Aidha, ninamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kutupatia ulinzi wake dhidi ya janga linaloisumbua dunia kwa sasa la mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na Virusi vya Corona (UVIKO).

3. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Watanzania wana imani na matumaini makubwa nae na kuwa chini ya uongozi wake nchi yetu itapiga hatua kubwa zaidi za kimaendeleo. Tunamtakia kila la kheri katika uongozi wake na kumuomba Mwenyezi Mungu azidi kumpa afya njema, hekima na maarifa kwa ajili ya kuiongoza nchi yetu.

4. ***Mheshimiwa Spika***, ninampongeza Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango kwa kuteuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hatimaye kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu, kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunaamini kuwa uzoefu wake katika uongozi utakuwa chachu katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake. Vilevile, ninampongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na makini, akiwa msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali hapa Bungeni.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa naomba kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwako wewe binafsi na Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kwa ujumla, kwa msiba mkubwa kwa Taifa letu wa kuondokewa na mpendwa wetu na kipenzi cha Watanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyeaga dunia tarehe 17 Machi, 2021. Kuondokewa na Jemedari wetu mahiri ni pigo kubwa si kwa Tanzania tu, bali pia ni pigo kwa Afrika Mashariki, Bara la Afrika na Dunia nzima kwa ujumla. Kipekee kwa Wizara ninayoiongoza, tumepata pigo kubwa kwani Hayati Magufuli alianzisha miradi mikubwa ya kimkakati na kuhakikisha inatekelezwa kwa mafanikio makubwa. Ninaendelea kumuomba Mwenyezi Mungu ampe pumziko la milele, Amina.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, naomba kutoa pole zangu kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Benjamin William Mkapa; aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Maalim Seif Sharif Hamad na Balozi Mhandisi John William Herbert Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Aidha, naomba nitoe pole nyingi kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara na Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditiye, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe. Tutaendelea kuwakumbuka kwa michango yao katika maendeleo na ustawi wa nchi yetu. Mwenyezi Mungu awape pumziko la milele, Amina.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nikupongeze na kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, Katibu wa Bunge, Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano ninaoendelea kuupata wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa mbalimbali kuhusu Wizara ninayoisimamia. Ninapenda kuwahakikishia kuwa, Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kufikia malengo ya Kisekta na Kitaifa kwa ujumla.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninapenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mhe. Seleman Moshi Kakoso (Mb), Mbunge wa Mpanda Vijijini na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Anne Killango Malecela (Mb), Mbunge wa Same Mashariki. Nakiri kuwa Wizara imenufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati hiyo katika kuchambua, kushauri na kufuatilia maendeleo ya Sekta za Ujenzi na Uchukuzi. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo yamezingatiwa katika Bajeti hii.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuwasilisha Hotuba hii, ninapenda kuwashukuru Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba zao zilizotangulia. Hotuba hizo zimeeleza kwa ujumla maendeleo ya sekta za Kijamii na Kiuchumi kwa mwaka 2020/21 na mwelekeo kwa mwaka 2021/22. Ninawashukuru na kuwapongeza pia Mawaziri wote waliowasilisha hotuba zao.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba sasa kuwasilisha hotuba yangu ambayo imejikita katika Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2020/21 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2021/22.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

### B-1 SEKTA YA UJENZI (FUNGU – 98)

11. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Sekta ya Ujenzi ilitengewa jumla ya Shilingi **38,774,425,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi Aprili, 2021 jumla ya **Shilingi 27,607,504,049.69,** sawa na asilimia **71.2** ya fedha zilizoidhinishwa zilikuwa zimetolewa na HAZINA kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

**Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa miradi ya maendeleo, katika mwaka wa fedha 2020/21, Sekta ya Ujenzi ilitengewa **Shilingi 1,577,586,781,000.00**. Kiasi hicho kinajumuisha **Shilingi 1,252,222,598,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 325,364,183,000.00** fedha za nje. Fedha za ndani zilijumuisha fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Funds) **Shilingi 610,476,228,000.00** na fedha za Mfuko wa Barabara **Shilingi 641,746,370,000.00.**

Hadi Aprili, 2021 fedha zilizopokelewa

ni **Shilingi 1,060,741,508,270.64,** sawa na asilimia **67.2** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 768,538,345,231.27** ni fedha za ndani na **Shilingi 292,203,163,039.37** ni fedha za nje.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**Miradi ya Barabara na Madaraja**

***13. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilipanga kutekeleza miradi ya barabara kuu inayohusisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa **kilometa 455.75** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja **11** pamoja na ukarabati wa **kilometa 25** kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia Aprili, 2021, jumla ya **kilometa 423.11** za barabara kuu zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya **kilometa 5.5** za barabara kuu zimekarabatiwa kwa kiwango cha lami. Aidha, utekelezaji wa miradi ya madaraja umekamilika kwa asilimia **36.36** ya mpango.

**14. Mheshimiwa *Spika,*** kwa upande wa barabara za mikoa, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia TANROADS ilipanga kujenga kwa kiwango cha lami barabara zenye urefu wa **kilometa 64.72** ambapo **kilometa 41.31** zilipangwa kujengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 23.41** zilipangwa kujengwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, **kilometa 1,005.33** zilipangwa kukarabatiwa kwa kiwango cha changarawe ambapo kati ya hizo, **kilometa 589.31** na madaraja **24** yalipangwa kukarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 416.2** na madaraja **27** yalipangwa kujengwa/kukarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.
Hadi Aprili, 2021 jumla ya kilometa **23.88** za barabara za mikoa zilijengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya kilometa **428.44** zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe. Aidha, utekelezaji wa miradi ya madaraja umekamilika kwa asilimia **23.14** ya mpango. Utekelezaji wa miradi uliathiriwa na kuchelewa kupatikana kwa misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Hata hivyo, Wizara ya Fedha na Mipango imeandaa Mfumo utakaorahisisha upatikanaji wa misamaha hiyo ya kodi.

***15. Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya miradi mikubwa ya barabara ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa ambayo ninapenda niitaje hapa ni pamoja na ujenzi wa barabara ya njia nane kutoka Kimara hadi Kibaha yenye urefu wa kilometa 19.2 ambayo ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 87.38 na ujenzi wa barabara ya mzunguko ya Dodoma (Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road) yenye urefu wa kilometa 112.3 ambayo makandarasi tayari wako eneo la ujenzi kwa ajili ya kuanza kazi. Miradi mingine ya ujenzi wa barabara inayoendelea ni kama ilivyoainishwa kwenye kitabu changu cha hotuba.

***16. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, Wizara ilipanga kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa ambayo yanahusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa kilometa **34,268.29,** matengenezo ya muda maalum kilometa **4,886.67** matengenezo ya sehemu korofi kilometa **743.49** na matengenezo ya madaraja **3,390.** Mpango huu pia unajumuisha shughuli za udhibiti wa uzito wa magari na ulinzi wa hifadhi za barabara, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu. Hadi Aprili, 2021 utekelezaji wa matengenezo katika barabara kuu na za mikoa ulikuwa umekamilika kwa asilimia **30.**

***17. Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa mradi wa **Ujenzi wa Madaraja Makubwa** umeendelea ambapo hadi Aprili, 2021, miradi iliyokamilika ni pamoja na ujenzi wa Daraja la Sibiti, Daraja la Magufuli (Kilombero), Daraja la Momba, Daraja la Mlalakuwa, Daraja la Magara, Daraja la Lukuledi na Daraja la Mara. Miradi mingine iliyokamilika ni Usanifu wa kina wa daraja la Simiyu, Daraja la Mitomoni na Daraja la Sanza. Aidha, Benki ya Dunia imeonesha nia ya kugharamia ujenzi wa daraja la Simiyu kupitia Mpango wa 'Lake Victoria Transport Programme'. Miradi mingine mikubwa ya madaraja inayoendelea ni Pamoja na ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi, Daraja Jipya la Wami, Daraja jipya la Selander, Daraja Jipya la Gerezani na ujenzi wa sehemu ya juu (deck) ya Daraja la Ruhuhu ambalo ujenzi wa msingi na nguzo umekamilika.

***18. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TANROADS iliendelea na kazi ya kudhibiti uzito wa magari kwa mujibu wa Sheria ya Afrika Mashariki ya Udhibiti wa Uzito wa Magari ya Mwaka 2016 na Kanuni zake za mwaka 2017 kwa kutumia jumla ya mizani **85**. Aidha, kati ya hiyo, mizani **63** ni ya kudumu na **22** ni inayohamishika. Kati ya mizani ya kudumu, mizani **13** ni ile inayopima uzito wakati magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion-WIM). Hadi kufikia Aprili, 2021, magari **4,465,261** yalikuwa yamepimwa ambapo kati ya hayo, magari **34,135** yalikuwa yamezidisha uzito zaidi ya asilimia tano (5) ya uzito unaoruhusiwa. Jumla ya **Shilingi 3,683,000,000.00** zilikusanywa kutokana na tozo ya uharibifu wa barabara. Katika kuongeza uwazi na uwajibikaji na hivyo kupunguza mianya ya rushwa, Wizara imeweka mifumo ya kamera katika mizani 13 na inaendelea kuweka mifumo hiyo katika mizani 42 nchi nzima. Aidha, Wizara inaendelea na utoaji wa vibali vya usafirishaji barabarani wa mizigo maalum nchini. Hadi Aprili, 2021 jumla ya **Shilingi 3,416,812,534.00** zilikusanywa kutokana na tozo ya upitishaji wa mizigo maalum.

*(Utekelezaji wa miradi ya Barabara na Madaraja umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba (**Ukurasa wa 10 hadi wa 49; Aya ya 18 hadi 102 pamoja na Aya ya 105**)*

**Vivuko na Majengo ya Serikali**

***19. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) iliendelea kutekeleza miradi ya *ujenzi na ukarabati wa maegesho ya vivuko***.**

Hadi Aprili, 2021 upanuzi wa jengo la abiria katika maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni Jijini Dar es Salaam ulikuwa katika hatua za mwisho. Vilevile, ujenzi wa miundombinu (jengo la abiria, ofisi na uzio) katika vituo kumi (10) vya vivuko uko katika hatua za manunuzi. Aidha, ujenzi wa maegesho ya Bukondo na Zumacheli katika kivuko cha Chato – Nkome upande wa Bukondo umekamilika na upande wa Zumacheli upo katika hatua za manunuzi. Ujenzi wa maegesho ya Nyamisati – Mafia umekamilika upande wa Nyamisati na upande wa Mafia ujenzi unaendelea kwa kutekelezwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Ukarabati wa maegesho ya vituo vinne (4) vya vivuko (Bugolora - Ukara, Rugezi - Kisorya, Nyakarilo - Kome na Kigongo – Busisi) umekamilika na maegesho ya Iramba – Majita yapo katika hatua za manunuzi. Aidha, maegesho ya Kayenzi - Kanyinga na Muleba – Ikuza yapo katika hatua ya upembuzi yakinifu.

***20. Mheshimiwa Spika,*** katika miradi ya ***ununuzi wa vivuko,*** hatua iliyofikiwa hadi kufikia Aprili, 2021 ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa vivuko vipya vya Nyamisati – Mafia, Chato - Nkome na Bugolora - Ukara. Aidha, ujenzi wa kivuko kipya cha Kisorya – Rugezi na ununuzi wa *fiber* boti mpya moja (1) kwa ajili ya kivuko cha Utete – Mkongo upo katika hatua za manunuzi.

***21. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu miradi ya ***Ukarabati wa Vivuko,*** iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/21, hadi Aprili, 2021 ukarabati mkubwa wa vivuko vya MV Kigamboni na MV Sengerema ulikuwa umekamilika na vinafanya kazi. Ukarabati wa MV Tegemeo, MV KIU na MV Misungwi unaendelea. Aidha, miradi ya ukarabati wa vivuko vya MV Musoma, MV Mara, MV Ujenzi, MV Kome II, MV Nyerere na MV Kilombero II ipo katika hatua mbalimbali za manunuzi.

***22. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) iliendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali. Hadi Aprili, 2021, kazi za ujenzi wa nyumba 5 za Majaji katika mikoa ya Kilimanjaro, Shinyanga, Mtwara, Dar es Salaam na Tabora zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, ujenzi wa nyumba za makazi Magomeni Kota umefikia asilimia 94. Vilevile, ukarabati wa nyumba za Viongozi 272 zilizopo Dodoma, 82 Dar es Salaam na 130 za watumishi wa umma mikoani zilizohamishiwa TBA toka TAMISEMI katika Mikoa 20 unaendelea ukiwa katika hatua za ukamilishaji.

*(Utekelezaji wa miradi ya Vivuko na Majengo umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 49 hadi wa 51; Aya ya 106 hadi ya Aya 110).***

**Viwanja vya Ndege**

***23. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia TANROADS imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege mbalimbali nchini ikiwemo viwanja vya Ndege vya Kigoma, Songwe, Tabora, Shinyanga, Sumbawanga, Mwanza, Arusha, Bukoba na Msalato. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ukarabati wa njia za kutua na kuruka, uwekaji wa taa na mitambo ya kuongezea ndege, ujenzi wa majengo ya uchunguzi wa hali ya hewa, Majengo ya abiria na kazi nyingine zinazohusiana na kuweka mazingira salama kwa abiria na ndege

*(Utekelezaji wa miradi ya Viwanja vya Ndege umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 53 hadi wa 59; Aya ya 114 hadi Aya ya 128).***

**Bodi ya Mfuko wa Barabara**

***24. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Mfuko wa Barabara ulitarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 916,780,529,000** kwa ajili ya kugharamia kazi za matengenezo na maendeleo ya barabara. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 641,746,370,000** zilikuwa kwa ajili ya kugharamia kazi za matengenezo na maendeleo ya barabara za Kitaifa (Barabara Kuu na Barabara za Mikoa). Aidha, **Shilingi 275,034,159,000** zilitengwa kwa ajili ya kugharamia kazi za matengenezo na maendeleo ya barabara za Wilaya kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Kati ya fedha hizo, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) ilitengewa **Shilingi 63,622,735,121.80,** Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilitengewa **Shilingi 27,266,886,523.26,** TANROADS ilitengewa **Shilingi 572,604,616,096.20,** TARURA ilitengewa Shilingi **245,401,978,709.34** na **Shilingi 7,884,312,549.40** zilitengwa kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

***25. Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2021 Bodi imekusanya na kugawanya jumla ya **Shilingi 716,813,813,708.00,** sawa na asilimia **78.19** ya bajeti ya mwaka. Kati ya hizo, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) ilipokea **Shilingi 49,745,445,017.00,** Ofisi ya Rais – TAMISEMI **Shilingi 21,289,561,708.00,** TANROADS **Shilingi 447,709,005,153.00,** TARURA **Shilingi 191,888,410,676.00** na Bodi ya Mfuko wa Barabara **Shilingi 6,189,381,154.00**

*(Utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Ujenzi umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 59 hadi wa 75; Aya ya 129 hadi Aya ya 155)***

**B-2 SEKTA YA UCHUKUZI (FUNGU – 62)**

***26. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 3,152,858,739,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, **Shilingi 3,062,148,630,000.00** ni fedha za Maendeleo na **Shilingi 90,710,109,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

**Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

***27. Mheshimiwa Spika***, katika bajeti ya mwaka 2020/2021, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa **Shilingi 90,710,109,000.00** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 63,639,165,000.00** ni fedha za Mishahara na **Shilingi 27,070,944,000.00** ni fedha za Matumizi Mengineyo kwa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Uchukuzi. Hadi kufikia Aprili, 2021, fedha za Matumizi ya Kawaida zilizotolewa kwa Sekta ya Uchukuzi na Taasisi zake ni **Shilingi 74,184,903,187.70** sawa na **asilimia 81.78** ya bajeti iliyoidhinishwa.

**Bajeti ya Maendeleo**

***28. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Sekta ya Uchukuzi ilitengewa jumla ya **Shilingi 3,062,148,630,000.00** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, **Shilingi 2,937,678,920,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 124,469,710,000.00** ni fedha za nje. Hadi kufikia Aprili, 2021 jumla ya fedha zilizotolewa ni **Shilingi 1,706,818,762,216.91** sawa na **asilimia 55.7** ya bajeti iliyoidhinishiwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,609,663,552,216.91** ni fedha za ndani sawa na **asilimia 54.8** ya bajeti iliyoidhinishwa na **Shilingi 97,155,210,000.00** ni fedha za nje sawa **asilimia 78.1** ya bajeti ya fedha za nje iliyoidhinishwa.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**Udhibiti wa Usafiri kwa Njia ya barabara**

***29. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeendelea kusimamia na kudhibiti usafiri katika sekta ndogo za reli, barabara na usafiri wa waya. Aidha, Mamlaka imeendelea kufuatilia mwenendo wa mabasi ya masafa marefu na treni (Vehicle Tracking System - VTS) ili kuimarisha shughuli za udhibiti wakati wote na mahali popote vyombo hivi vilipo. Hadi Aprili, 2021, jumla ya mabasi 5,386 na vichwa vya treni vitano (5) vilikuwa vimeunganishwa kwenye mfumo huo.

***30. Mheshimiwa Spika,*** kazi ya uunganishaji wa mabasi kwenye mfumo wa tiketi za kielektroniki (Electronic Ticketing System) inaendelea. Hadi sasa jumla ya mabasi 2,194 kati ya mabasi 5,386 sawa na asilimia 40 ya mabasi yote yanayotoa huduma za usafiri mikoani yameunganishwa katika mfumo wa tiketi mtandao. Matumizi ya mfumo huu yatasaidia kupata takwimu sahihi za watumiaji wa huduma, kuondoa changamoto ya wapiga debe kwenye vituo vya mabasi, kupunguza gharama za uendeshaji kwa watoa huduma na kusimamia mapato ya Serikali. Aidha, abiria wataweza kupata huduma popote walipo hivyo kupunguziwa gharama na muda wa kufuata tiketi kwa mawakala wa mabasi hayo. Napenda kutumia fursa hii kuwasihi Wamiliki wa Mabasi na Chama chao kuendelea kushirikiana na LATRA ili kutatua changamoto katika matumizi ya mifumo ya TEHAMA.

*(Utendaji katika udhibiti wa usafiri kwa njia ya barabara katika mwaka 2020/2021 umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 77 hadi wa 80; Aya ya 159 hadi Aya ya 164)***

**Shirika la Reli Tanzania (TRC)**

***31. Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Reli Tanzania (TRC) limeendelea kusimamia, kuboresha na kuendeleza miundombinu na huduma za usafiri wa reli yenye jumla ya urefu wa Kilometa 2,706 kwa ajili ya kuhudumia nchi jirani za Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, TRC ilisafirisha tani za mizigo 257,602 ikilinganishwa na tani 249,960 zilizosafirishwa kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya abiria wa masafa marefu 333,696 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 369,638 waliosafirishwa kipindi kama hicho katika mwaka 2019/20. Sababu za upungufu huu ni athari za mlipuko wa COVID19 na kufungwa kwa njia kutokana na ajali.

***32. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, Serikali imeendelea kusimamia ujenzi wa reli ya Dar es Salaam hadi Mwanza kwa kiwango cha *Standard Gauge* (SGR). Ujenzi wa reli ya Kati kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro (km 300) umekamilika kwa asilimia 91. Kuhusu kipande cha reli kutoka Morogoro hadi Makutupora (km 422), ujenzi unaendelea na umekamilika kwa asilimia 60.2. Aidha, kazi za ujenzi wa mfumo wa umeme katika Mradi wa SGR imekamilika kwa asilimia 100 kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro na asilimia 35.62 kwa kipande cha Morogoro hadi Makutupora. Pia, Tarehe 8 Januari 2021, Serikali kupitia TRC ilisaini Mkataba na ubia wa kampuni za *China Civil Engineering Construction Corporation* (CCECC) na *China Railway Construction Corporation Limited* (CRCC) za China kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Mwanza-Isaka (Km 341). Malipo ya awali (advance payments) ya ujenzi wa kipande hiki ya Shilingi bilioni 376.44 yamefanyika Aprili, 2021. Kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Mei, 2021 na sasa Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya ujenzi ikiwemo uletaji wa mitambo.

***33. Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na majadiliano na Taasisi za fedha na Washirika wa Maendeleo mbalimbali walioonesha nia ya kugharamia ujenzi wa reli ya SGR vipande vya Makutupora – Tabora (km 294) na Tabora – Isaka (km 133). Maeneo mengine yanayoendelea kutafutiwa fedha za ujenzi ni pamoja na Tabora – Kigoma (km 411), Keza - Ruvubu (km 36), Uvinza-Musongati (km 200), Kaliua – Mpanda - Karema (km 321) na Isaka - Rusumo (km 371).

***34. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ununuzi wa vifaa vya uendeshaji wa Reli ya SGR, Mkataba wa ununuzi wa Vichwa viwili (2) vya Treni za umeme pamoja na Mabehewa 30 ulisainiwa Oktoba, 2020. Majaribio ya kwanza ya Reli ya SGR yamepangwa kufanyika Agosti, 2021.

*(Utekelezaji wa miradi ya reli ya Kati kupitia TRC umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 81 hadi wa 86 Aya ya 168 hadi Aya 177**).*

**Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)**

***35. Mheshimiwa* Spika,** huduma za kusafirisha abiria na mizigo kwa njia ya reli kati ya Dar es Salaam, Tanzania na New Kapiri Mposhi, Zambia zimeendelea kutolewa na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (Tanzania Zambia Railway Authority - TAZARA). Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, TAZARA ilisafirisha jumla ya tani 167,242 za mizigo ikilinganishwa na tani 148,681 zilizosafirishwa kwa kipindi kama hicho 2019/2020. Ongezeko hili limechangiwa na kuanza kufanya kazi kwa Injini saba (7) zilizofungwa vipuri vipya vilivyonunuliwa na Serikali pamoja na matengenezo ya njia ya reli hasa kwenye maeneo korofi. Treni hizi kwa sasa zinafanya safari kati ya Dar es salaam na Mbeya kwa upande wa Tanzania na kati ya Nakonde na New Kapiri Mposhi kwa upande wa Zambia

*(Utekelezaji wa miradi ya reli ya TAZARA umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 87 hadi wa 89 aya ya 178 hadi 182**)*

**Udhibiti wa Huduma za Usafiri kwa njia ya Maji**

***36. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (Tanzania Shipping Agencies Corporation - TASAC) imeendelea kudhibiti ulinzi na usalama wa vyombo vya usafiri kwa njia ya maji na kudhibiti uchafuzi wa mazingira majini utokanao na shughuli za usafiri kwa njia ya maji. Pia, Shirika limeendeleza na kupanua huduma za sekta ya usafiri kwa njia ya maji; kudhibiti huduma za bandari na usafiri kwa njia ya maji; na kuhimiza ufanisi, uchumi na ushindani katika biashara ya uwakala wa Meli. Aidha, TASAC imeendelea kufanya kazi za uwakala wa Meli kwa nia ya kulinda maslahi mapana ya nchi.

***37. Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kukagua utendaji wa bandari nchini na usafiri wa meli kwa lengo la kujiridhisha na uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, viwango vya huduma, na utoshelevu wake kwa wateja na kutoa miongozo kwa kuzingatia viwango vya kimataifa. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, Kituo cha kuratibu shughuli za utafutaji na uokoaji Majini (Maritime Rescue Coordination Centre - MRCC) kilichopo Dar es Salaam kilipokea taarifa za ajali nne (4) za vyombo vya usafiri kwa njia ya maji ambazo zilitokea katika maeneo ya maji yaliyomo Tanzania Bara. Ajali hizo zilihusisha jumla ya watu 136; ambapo kati yao watu 20 walipoteza maisha na watu 116 waliokolewa. Aidha, Kituo kilipokea jumla ya taarifa za matukio (maritime distress) 11 yaliyohusisha jumla ya watu 50, ambao wote waliokolewa. *(Utendaji katika udhibiti wa usafiri kwa njia ya maji kwa mwaka 2020/2021 umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 89 hadi wa 92, Aya ya 183 hadi 188**)*

**Huduma za Uchukuzi katika Maziwa**

***38. Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Huduma za Meli (Marine Services Company Limited - MSCL) imeendelea kutoa huduma ya usafiri wa abiria na mizigo katika maziwa makuu ya Tanganyika, Victoria na Nyasa. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, Kampuni ilisafirisha jumla ya abiria 220,122 ikilinganishwa na abiria 55,053 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2019/2020. Kuongezeka kwa abiria kumetokana na kuanza kutoa huduma kwa Meli mbili za New Victoria *Hapa Kazi Tu* na New Butiama *Hapa Kazi Tu* baada ya kufanyiwa ukarabati mkubwa na kuanza kutoa huduma katika Ziwa Victoria mwezi Agosti, 2020. Utendaji huu uliiwezesha MSCL kukusanya jumla ya shilingi bilioni 3.58 ikilinganishwa na Shilingi milioni 897.86 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020.

***39. Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya MSCL imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Meli moja (1) mpya ya kubeba abiria na mizigo pamoja na Chelezo katika Ziwa Victoria. Aidha, MSCL iliendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa meli katika Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria pamoja na Ujenzi wa Meli mpya ya Mizigo katika Bahari ya Hindi. Hadi kufikia Aprili, 2021, Ujenzi wa Meli mpya MV Mwanza *Hapa Kazi Tu* yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo ulikamilika kwa asilimia 69.5 na utakamilika Disemba, 2021.

*(Utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli zilizopo katika maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 93 hadi wa 96 Aya ya 191 hadi 193**)*

**Huduma za Bandari**

***40. Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (Tanzania Ports Authority - TPA) imeendelea kumiliki Bandari za Mwambao na za Maziwa. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, TPA ilihudumia shehena ya tani za mapato milioni 9.97 ikilinganishwa na shehena ya tani za mapato milioni 10.42 iliyohudumiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2019/2020. Aidha, jumla ya magari 107,869 yalipakuliwa katika Bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na magari 125,758 yaliyopakuliwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2019/2020. Sababu za kushuka kwa utendaji huu ni pamoja na athari za mlipuko wa COVID-19 uliosababisha mdodoro wa shughuli za usafirishaji kwa njia ya maji duniani pamoja na uchache wa vifaa na mitambo ya kuhudumia shehena bandarini.

***41. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPA inaendelea na uboreshaji wa Bandari za Mwambao wa Bahari ya Hindi za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara pamoja na bandari zilizopo kwenye Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Kuhusu ujenzi wa Gati la kupokelea mafuta kutoka Uganda lililoko eneo la Chongoleani, maandalizi ya ujenzi wa Gati hilo yanaendelea wakati majadiliano ya utekelezaji wa mradi huu baina Tanzania na Uganda yakiwa

yanaendelea kukamilishwa.

*(Utekelezaji wa miradi ya uboreshaji wa bandari zilizo kwenye mwambao wa bahari ya Hindi na Maziwa Makuu umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 96 hadi wa 102; Aya ya 194 hadi 201)***

**Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Anga**

***42. Mheshimiwa Spika,*** udhibiti wa huduma za usafiri wa anga, viwanja vya ndege, masuala ya kiusalama na kiuchumi katika usafiri wa anga na utoaji wa huduma za uongozaji ndege umeendelea kufanywa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga (Tanzania Civil Aviation Authority - TCAA). Mamlaka hii pia imeendelea kudhibiti Viwanja vya Ndege vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA), Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Sekta Binafsi. Lengo ni kuimarisha utoaji huduma, kukuza utalii nchini na kuendelea kuhakikisha utekelezaji wa Sheria na Kanuni za uendeshaji wa Viwanja vya Ndege.

***43. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, idadi ya Abiria wanaotumia usafiri wa anga imepungua hadi kufikia abiria 2,495,379 ikilinganishwa na abiria 4,423,732 waliotumia usafiri huo katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/2020. Aidha, idadi ya Abiria wanaosafiri ndani ya nchi imepungua hadi abiria 1,676,107 ikilinganishwa na Abiria 2,342,059 waliosafiri katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Idadi ya Abiria wanaosafiri kwenda na kutoka nje ya nchi imepungua kutoka abiria 2,081,673 hadi kufikia abiria 819,272. Sababu za kupungua kwa abiria wanaosafiri ndani na nje ya nchi ni mlipuko wa ugonjwa wa COVID 19 ambapo nchi nyingi zilifunga na kuzuia safari za anga.

**Huduma za Viwanja vya Ndege**

***44. Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) imeendelea kutoa huduma kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Usafiri wa Anga. Mamlaka hii ina jukumu la kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege 59 vinavyomilikiwa na Serikali isipokuwa vilivyo chini ya Mamlaka za Hifadhi, Halmashauri, Jeshi na Taasisi binafsi. Katika utekelezaji wa majukumu yake, TAA imeendelea kusimamia shughuli za uendeshaji wa Jengo jipya la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere.

***45. Mheshimiwa Spika,*** uendelezaji na uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) umeendelea kusimamiwa na Kampuni ya Kuendeleza Viwanja vya Ndege ya Kilimanjaro (KADCO). Kampuni hii imeendelea kuhakikisha kuwa inahudumia mizigo inayohitaji ubaridi (Cold Storage Facility) ili kuvutia biashara ya usafirishaji wa mizigo mbalimbali kama vile mbogamboga, matunda na maua kupitia Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro. Hivyo, napenda kutumia fursa hii kuwasihi na kuwakaribisha wafanyabiashara wa mbogamboga, minofu ya nyama na samaki, matunda na maua kutumia kiwanja cha KIA kwani huduma za kuhifadhi mizigo kwenye ubaridi zinapatikana.

**Huduma za Usafiri wa Anga**

***46. Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Ndege ya Tanzania (Air Tanzania Company Limited - ATCL) imeendelea kutoa huduma za kusafirisha abiria na mizigo ndani na nje ya Tanzania. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, Serikali ilinunua ndege mbili (2) aina ya A220-300 na ndege moja aina ya Dash 8 Q400. Utengenezaji wa Ndege hizo haukukamilika kwa muda uliopangwa kutokana na athari za mlipuko wa COVID-19 uliosababisha viwanda kusimamisha uzalishaji. Kati ya ndege hizo, ndege moja aina ya Dash 8 Q400 inatarajiwa kuwasili nchini Juni, 2021 na ndege nyingine mbili aina ya Airbus (A220-300) zinatarajiwa kuwasili nchini mwezi Agosti, 2021 na Oktoba, 2021.

*(Maelezo kuhusu utendaji katika usafiri na uchukuzi kwa njia ya anga kwa mwaka 2020/21 yametolewa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 103 hadi wa 115; Aya ya 202 hadi 224)***

**Huduma za Hali ya Hewa**

***47. Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) imeendelea kusimamia, kudhibiti na kuratibu utoaji wa huduma za hali ya hewa hapa nchini. Utoaji wa huduma za hali ya hewa nchini umeendelea kuwa bora ambapo usahihi wa utabiri umefikia asilimia 87.9. Kiwango hiki ni juu ya kiwango kinachokubalika na Shirika la Hali ya Hewa Duniani ambacho ni asilimia 70. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, kazi ya ufungaji wa rada ya hali ya hewa huko Mtwara ilikamilika na kukabidhiwa Disemba, 2020. Aidha, malipo ya ununuzi wa Rada mbili (2) za hali ya hewa zitakazofungwa Mbeya na Kigoma yamekamilika kwa asilimia 90 na utengenezaji uko katika hatua za mwisho.

*(Utekelezaji wa miradi na huduma za hali ya hewa umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 115 hadi wa 117; Aya ya 225 hadi 227)***

**TAASISI ZA MAFUNZO**

***48. Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa majukumu ya Taasisi za Mafunzo zinazosimamiwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba kuanzia ***Ukurasa wa 117 hadi wa 124;* Aya ya 228 hadi Aya ya 240.**

**C. CHANGAMOTO ZILIZOIKABILI WIZARA NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAZO**

***49. Mheshimiwa Spika***, katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imekabiliwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo na mikakati ya kukabiliana nayo imeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba ***Ukurasa wa 129 hadi wa 136; Aya ya 249.***

**D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA SEKTA ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22**

***50. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2021/22 kwa kuzingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020.

**D.1.1 SEKTA YA UJENZI**

**Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo**

***51. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2021/22, Sekta ya Ujenzi (Fungu 98) imetengewa jumla ya **Shilingi 1,627,244,274,200.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekta ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2021/22 ni **Shilingi 38,540,787,000.00.** Kati ya hizo, **Shilingi 35,186,389,000.00** ni Bajeti ya Mishahara na **Shilingi 3,354,398,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Sekta ya Ujenzi imetengewa jumla ya **Shilingi 1,588,703,487,200.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,288,703,487,200.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 300,000,000,000.00** ni za fedha za nje. Kati ya fedha za ndani **Shilingi 635,849,127,200.00** zimetengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara na fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni **Shilingi 652,854,360,000.00.**

*Mgawanyo wa fedha za maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyoonyeshwa katika **Viambatisho Na.1 na Na. 2 vya Hotuba.***

**FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA**

***52. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi 635,849,127,200.00** kutoka Mfuko wa Barabara zimetengwa kwa ajili ya kufanya kazi za matengenezo na

ukarabati wa barabara kuu na za mikoa. Kati ya fedha hizo, TANROADS imetengewa **Shilingi 567,342,742,235.00** kwa ajili ya matengenezo ya barabara na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) imetengewa **Shilingi 63,038,082,471.00** kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara za mikoa, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko, usalama barabarani pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo. Aidha, **Shilingi 5,468,302,494.00** zitatumika kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

***53. Mheshimiwa Spika,*** mgawanyo wa **Shilingi 63,038,082,471.00** zilizotengwa kwa ajili ya Wizara (Ujenzi) ni kama ifuatavyo: **Shilingi 16,784,830,349.00** ni kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara zenye urefu wa kilometa **5,310; Shilingi 4,740,226,000.00** ni kwa ajili ya manunuzi na ukarabati wa vivuko pamoja na ujenzi wa maegesho ya vivuko; **Shilingi 4,161,577,576.00** ni kwa ajili ya miradi ya Usalama Barabarani na Mazingira na **Shilingi 4,738,982,546.00** ni kwa ajili ya kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara (Ujenzi) pamoja na kujenga uwezo wa watumishi. Aidha, **Shilingi 32,612,466,000.00** zimetengwa kwa ajili ya miradi ya barabara za mikoa itakayohusisha ukarabati wa jumla ya kilometa **426** kwa kiwango cha changarawe, ujenzi wa kilometa **30.8** kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi na ukarabati wa madaraja/makalavati **32** katika mikoa mbalimbali nchini. *Mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi) umeonyeshwa katika **Viambatisho Na. 3 na 4.** Aidha, mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo umeoneshwa katika **Viambatisho Na. 5, 5A - 5D.***

**D.1.2 SEKTA YA UCHUKUZI**

**Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo**

***54. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62) imetengewa jumla ya **Shilingi 2,120,049,821,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 91,743,411,000.00** zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,028,306,410,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Katika Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotengwa, **Shilingi 1,828,306,410,000.00** ni fedha za Ndani na **Shilingi 200,000,000,000.00** ni fedha za Nje. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na.6.** Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 64,672,467,000.00** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 27,070,944,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Sekta ya Uchukuzi na taasisi zake.

*(Mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa kwa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na Fedha za vyanzo vya ndani ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba kuanzia **Aya ya 410 hadi Aya ya 423** pamoja na **Aya 425 hadi Aya ya 426** kwa Taasisi za Mafunzo chini ya Sekta ya Uchukuzi)*

**E. SHUKRANI**

***55. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwashukuru wananchi na wadau mbalimbali hasa sekta binafsi kwa ushirikiano wao katika kutekeleza malengo ya Sekta zetu. Shukurani za pekee ziwaendee Waheshimiwa wabunge wenzangu kwa michango yao ambayo imechangia katika kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara. Naomba waendelee na moyo huo ili tuweze kuendeleza Wizara hii ambayo ni muhimu katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

***56. Mheshimiwa Spika,*** shukurani zangu hazitakuwa kamili bila kuwashukuru Viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa ***Mhandis**i* **Godfrey Msongwe Kasekenya (Mb.)** na Mheshimiwa **Mwita Mwikwabe Waitara (Mb.);** Makatibu Wakuu ***Mhandisi*** **Joseph Kizito Malongo** (Ujenzi) na Bwana **Gabriel Joseph Migire** (Uchukuzi). Aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara, Viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, Watumishi na Wataalamu wote wa Wizara kwa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara. Naomba waendelee na juhudi hizo katika kipindi kijacho ili tuweze kutekeleza malengo Wizara na ya Taifa kwa ujumla.

***57. Mheshimiwa Spika,*** Washirika mbalimbali wa Maendeleo wamekuwa wakichangia katika utekelezaji wa Programu na Mipango mbalimbali ya Wizara. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwatambua Washirika hao wa Maendeleo ambao ni pamoja na Shirika la Kimataifa la Usafiri kwa njia ya Maji (IMO), Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO), Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA), *OPEC Fund*, Umoja wa Nchi za Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Japan (JICA), Korea Kusini (KOICA), *Abu Dhabi Fund*, Ujerumani (KfW), Uingereza (DFID), Uholanzi (ORIO), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Kuwait (KFAED), Uturuki, *HSBC*, *TMEA*, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC, Nchi za Urusi, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Uholanzi, Japan, India, China, Denmark, Norway, Ubelgiji, Ujerumani, Taasisi za fedha za CRDB, NSSF, PSSSF na TIB, Asasi zisizokuwa za Kiserikali; Sekta Binafsi pamoja na wengine wengi.

***58. Mheshimiwa Spika,*** mwisho, nakushukuru tena wewe binafsi na Mhe. Naibu Spika. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (**www.mwt.go.tz**).

**F. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

***59. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 3,747,294,095,200.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,627,244,274,200.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi na **Shilingi 2,120,049,821,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:

**F.1. SEKTA YA UJENZI (FUNGU 98)**

***60. Mheshimiwa Spika,*** **Shilingi 1,627,244,274,200.00** za Fungu 98 (Ujenzi) zinajumuisha **Shilingi 38,540,787,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara (Ujenzi) na Taasisi ambapo **Shilingi 35,186,389,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 3,354,398,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. Bajeti ya Maendeleo ni Shilingi **1,588,703,487,200.00** ambazo zinajumuisha **Shilingi 1,288,703,487,200.00** fedha za ndani na **Shilingi 300,000,000,000.00** fedha za nje. Fedha za ndani zinajumuisha **Shilingi 635,849,127,200.00** za Mfuko wa Barabara na **Shilingi 652,854,360,000.00** za Mfuko Mkuu wa Serikali.

**F.2. SEKTA YA UCHUKUZI (FUNGU 62)**

***61. Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uchukuzi imetengewa jumla ya **Shilingi 2,120,049,821,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, **Shilingi 91,743,411,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 64,672,467,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 27,070,944,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. Aidha, Miradi ya Maendeleo imetengewa **Shilingi 2,028,306,410,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,828,306,410,000.00** ni fedha za Ndani na **Shilingi 200,000,000,000.00** ni fedha za Nje.

***62. Mheshimiwa Spika***, pamoja na Hotuba hii, nimeambatanisha Miradi ya Wizara itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/22 **(Kiambatisho Na. 1-6)** ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza Miradi hiyo. Naomba kitabu kizima cha Hotuba yangu ya bajeti pamoja na viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya hoja hii.

***63. Mheshimiwa Spika***, Naomba kutoa hoja.

# Taasisi ya kilimo Kenya yavuliwa mamlaka sakata mahindi Tanzania

**Nairobi,** KENYA

WAZIRI wa Kilimo, Peter Munya ameipokonya mamlaka taasisi inayohusika na kutoa idhini ya kuingiza nafaka nchini Kenya katika maeneo ya mpaka (AFA).

Munya alisema serikali badala yake itaitumia Taasisi ya Ukaguzi wa Usalama wa Mazao (Kephis) kuhakikisha kuwa mahindi yana viwango vinavyohitajika.

"Kuanzia sasa, AFA haitasajili mahindi ambayo tayari yamesajiliwa na Kephis. Sisi sote tunahimiza kuchukuliwa sampuli moja wakati malori ya kampuni moja yanapoingiza bidhaa," alisema Munya, Ijumaa iliyopita wakati alipotembelea mpaka wa Namanga.Hatua hiyo inafuatia agizo la wiki iliyopita la Rais Uhuru Kenyatta, kwa waziri huyo kuhakikisha idhini ya kuingiza mahindi inapatikana haraka wakati wa ziara ya kiserikali ya siku mbili na mwenzake wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

Kenya ilipiga marufuku mara moja ununuzi wa mahindi kutoka mataifa jirani ya Tanzania na Uganda.

Kulingana na barua iliyoandikwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kilimo na Chakula, Kello Harsama kwa Pamela Ahago ambaye ni Kamishna wa forodha katika mamlaka ya ushuru Kenya (KRA), ununuzi huo ulisitishwa baada ya uchunguzi kubaini mahindi kutoka mataifa hayo mawili sio salama kwa matumizi ya chakula cha binadamu.

Mamlaka hiyo imekuwa ikifanya uchunguzi kuhusu usalama wa chakula kinachoingizwa nchini Kenya.

BBC



Baadhi ya majengo yaliyoko ukanda wa Gaza, yakiwa yameshambuliwa na mashambulizi ya angani kutoka Israel, jana. Mashambulizi hayo yanayotokana na mgogoro kati ya Israel na Palestina kwa kipindi cha wiki moja sasa yameshasababisha vifo vya watu 200. **PICHA: BBC**

# Vifo vyafikia 200 mashambulizi Gaza

**Gaza,** PALESTINA

ZAIDI ya vifo 200 vimeripotiwa kwa wiki moja tangu mashambulizi yanayoendelea ukanda wa Gaza.

Licha ya wito wa kusitisha mapigano yanaendelea kwa siku ya saba mfululizo, kati ya Israel na Palestina.

Kati ya chanzo cha mapigano hayo ni mvutano wa Israeli na Hamas.

Usiku wa juzi na mapema jana Israeli iliendelea kurusha makombora katika Ukanda wa Gaza kwa kutumia ndege za Israel.

Mamia ya majengo yaliharibiwa, kulingana na serikali za mitaa, ambazo hazikuripoti majeruhi wowote.

Jeshi la Israel, Tsahal, limetetea uamuzi wake wa kutekeleza mashambulizi hayo likidai kwamba linalenga magaidi bila kutoa maelezo zaidi.

Lakini Palestina, raia wake wanahofu kubwa ya kutokea maafa zaidi.

"Hakujawahi kutokea mashambulizi makubwa kama haya," alisema Mad Abed Rabbo, 39, ambaye anaishi katika Jiji la Gaza Magharibi.

"Nilihisi kama ninakufa," alisema mkazi mwingine kabla ya kuongeza, "lazima Netanyahu atambue kwamba sisi ni raia, sio wanajeshi."

Jumapili Jumuiya ya Ushirikiano wa Mataifa 57 ya Kiislamu ilikutana kwa dharura, kujadili mapigano makali yanayoendelea baina ya Israel na wanamgambo wa kundi la Hamas linalodhibiti Ukanda wa Gaza.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Mamlaka ya Palestina, Riad al-Malki, alilaani mashambulizi ya Israel aliyoyaita ya uoga wakati wa ufunguzi wa mkutano huo, akisema uhalifu unafanywa dhidi ya Palestina bila ya kuwapo na athari.

Hata hivyo Mamlaka ya Palestina haina udhibiti dhidi ya kundi la Hamas na ukanda wa Gaza, ambako wapiganaji walichukua mamlaka mwaka 2007.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uturuki, Mevlut Cavusoglu, alisema Israel pekee ndio yenye kuwajibika na machafuko ya karibuni huko Jerusalemu, Ukingo wa Magharibi na Ukanda wa Gaza.

RFI

# Ufaransa yaisaidia Sudan kulipa deni IMF

**Paris,** UFARANSA

UFARANSA imesema itaipatia Sudan mkopo wa dola bilioni 1.5, kwa lengo la kuisaidia kulipa deni lake kubwa inalodaiwa na Shirika la Kimataifa la Fedha (IMF).

Waziri wa Fedha wa Ufaransa, Bruno Le Maire alisema hayo jana, kwenye ufunguzi wa mkutano wa kimataifa unaolenga kulisaidia taifa hilo lililopo kwenye mchakato wa kujitoa kwenye utawala wa kiimla hadi wa kidemokrasia.

Waziri huyo wa fedha alisema, Rais Emmanuel Macron atathibitisha hatua hiyo.

Waziri Mkuu wa Sudan, Abdallah Hamdok anahudhuria mkutano huo unaofanyika mjini Paris, akisaka uungwaji mkono wakati taifa hilo likipambana kulipa deni la nje, linalofikia dola bilioni 60, pia akitaraji kupata makubaliano ya uwekezaji.

Hamdok anashinikiza ujenzi mpya na kuleta mabadiliko kwenye uchumi uliozorota, pia kuhitimisha hatua ya kutengwa kwa taifa hilo iliyochukuliwa katika enzi ya utawala wa Omar al-Bashir. Chini ya utawala wake wa miongo mitatu, taifa hilo liligubikwa na hali ngumu na vikwazo vya kiuchumi.

Hamdok aliliambia Shirika la habari la AFP, kabla ya mkutano huo kuwa, anaamini kwamba Sudan inaweza kukabiliana na deni hilo la nje, iwapo litafanikiwa kuingia mikataba ya uwekezaji na nafuu ya madeni.

Waziri huyo wa fedha wa Ufaransa, alisisitiza kwamba si suala la muda mfupi la kujenga upya uchumi, utakaovutia na endelevu na kuongeza, mkutano huo utawashawishi wawekezaji binafsi katika fursa muhimu za kibiashara nchini Sudan.

DW

## Zaidi ya 700,000 walikufa sababu ya saa nyingi za kazi

**Geneva,** USWISI

SAA nyingi za kazi ni sababu ya watu 745,000 kupoteza maisha mwaka 2016 kutokana na magonjwa ya kiharusi na moyo.

Hayo ni kwa mujibu wa mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN) na kwamba asilimia 72 ya vifo hivyo huwakumba wanaume, hasa katika Kanda ya Magharibi ya Pasifiki na Kanda za Kusini Mashariki mwa Asia. Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), pamoja na Shirika la Kazi Duniani (ILO), zilizochapishwa jana, zinakadiria kwamba watu 398,000 walikufa kwa kiharusi na wengine 347,000 kwa ugonjwa wa moyo.

Pia mashirika hayo yalibaini watu hufanya kazi kwa muda usiopungua saa 55 kwa wiki.

Kati ya mwaka 2000 na 2016, idadi ya vifo kutokana na maradhi ya moyo, yaliyosababishwa na kufanya kazi kwa saa nyingi, iliongezeka kwa asilimia 42, huku ile ya kiharusi, ikiongezeka kwa asilimia 19.

Kadhalika, ilifahamika kwamba kufanya kazi kwa saa 55 kwa wiki kunahusishwa na asilimia 35 ya hatari ya kupata kiharusi na asilimia 17 ya ugonjwa wa moyo, ikilinganishwa na kufanya kazi kati ya saa 35 hadi 40 kwa wiki.

DW

## Kesi ya Jacob Zuma yasogezwa mbele

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

KESI ya ufisadi ya Rais wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, imesogezwa hadi Mei 26, mwaka huu, ombi rasmi litakapowasilishwa.

Anatarajiwa kukana mashtaka yanayomkabili.


Wafuasi wa Zuma walikusanyika nje ya Mahakama Kuu ya Pietermaritzburg kabla yeye kujitokeza.

Rais huyo wa zamani anakabiliwa na makosa 16 ya ufisadi, unaohusiana na makubaliano ya silaha ya mabilioni ya dola.Jumla ya mashahidi 217 wanatarajiwa kutoa ushahidi dhidi yake.

Kesi hiyo inahusu makubaliano ya biashara ya silaha na kampuni ya silaha ya Ufaransa, Thales, ambayo ilikuwa na nia ya kuboresha ulinzi wa Afrika Kusini mwishoni mwa miaka ya 1990.

Zuma na kampuni hiyo, wamekana mashtaka ambayo ni pamoja na udanganyifu, ulaghai na uhujumu uchumi.

BBC




# MAGUIRE KUCHEZA FAINALI YA EUROPA - SOLSKJAER

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema Harry Maguire yupo kwenye hali "chanya" kuhusu nafasi yake ya kucheza fainali ya Ligi ya Europa.

Mlinzi huyo wa England anaendelea kujiuguza kifundo cha mguu na kumfanya kukosa mechi mbili za mwisho za Ligi Kuu England dhidi ya Fulham na Wolves.

United watacheza na Villarreal kwenye fainali ya Ligi ya Europa Mei 26 na Solskjaer ana matumaini nahodha wake huyo atakuwapo.

**"Anaonyesha ishara nzuri, tunahofu ya kuanza kumtumia mapema, lakini naamini tunaweza kuwa naye kwenye fainali kwa sababu maendeleo yake ni mazuri," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.**

"Anapenda sana kurudi uwanjani, lakini hataki kujiingiza kwenye hatari mapema. Wakati nilipozungumza naye, alikuwa anaonyesha hali chanya kabisa, nina matumaini makubwa.

"Lakini ni mapema sana kuamua kama atakuwapo, ingawa matumaini yetu ni makubwa kuwa naye kikosini."

## POCHETTINO BADO ANA MATUMAINI NA TAJI PSG

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA Mkuu wa Paris Saint-Germain, Mauricio Pochettino amesema timu yake lazima iamini kwenye nafasi yao ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, kwenye mechi ya mwisho ya msimu.

PSG iliweka matumaini yake wazi ya kutetea taji la ligi, shukrani kwa ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Reims Jumapili, na kuwafanya wapitwe pointi moja na vinara Lille kuelekea mchezo wa mwisho wa msimu huu wa 2020-21.

Neymar na Kylian Mbappe walikuwa kwenye orodha ya wafungaji dhidi ya Reims na PSG sasa itacheza na Brest kwenye mchezo wa mwisho, huku wakihitaji ushindi na kuwaombea Lille kufungwa na Angers.

Kwa sasa Lille wanapointi 80 huku PSG wakiwa na pointi 79, na bado kila moja ikibakiwa na mchezo mmoja kumaliza ligi hiyo.

"Kitu muhimu ni kuamini kuhusu nafasi yetu," alisema Pochettino akiwaambia waandishi wa habari.

"Lakini tunatakiwa kuangalia mchezo wetu wa Jumatano wa fainali ya Coupe de France dhidi ya Monaco.

"Hilo ndilo jukumu letu la kwanza. Halafu baada ya Fainali ya Ufaransa tutauangalia mchezo wetu wa mwisho dhidi ya Brest."



## HAALAND KUBAKIA DORTMUND MSIMU UJAO

**DORTMUND, Ujerumani**

ERLING Haaland atabaki kuwa mchezaji wa Borussia Dortmund msimu ujao, Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo ya Ujerumani, Michael Zorc amedai.

Klabu kama Real Madrid, Barcelona na Manchester City wamekuwa wakihusishwa sana na uhamisho wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 raia wa Norway.

Haaland alijiunga na Dortmund kutoka Salzburg katikati ya msimu wa 2019-20 na amefunga mabao mengi kwa klabu hiyo ya Bundesliga.

Mabao yake mawili yaliisaidia Dortmund kuifunga RB Leipzig 4-1 kwenye fainali ya Kombe la DFB-Pokal mjini Berlin Alhamisi, na bosi huyo wa BVB, ameelezea majaliwa ya nyota huyo.

Haaland ameripotiwa kwamba ana kipengele kwenye mkataba wake cha Euro milioni 75 ili kuondoka msimu ujao, huku mkataba wake ukiwa unamalizika mwaka 2024.

"Bado tuna mipango na yeye. Atacheza kwetu msimu ujao," alisema Zorc akiiambia Sky Sport Ujerumani.



# 'MESSI HAJACHEZA MECHI YA MWISHO CAMP NOU'

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman ana matumaini, Lionel Messi, hajacheza mechi ya mwisho kwenye klabu hiyo katika dimba la Camp Nou, lakini amekubali straika huyo hajapata sapoti ya kutosha msimu huu.

Messi alifunga bao lake la 30 kwenye ligi Jumapili wakati Barca ikifuta rasmi matumaini ya kuwania ubingwa wa LaLiga baada ya kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Celta Vigo kwenye mchezo wao wa mwisho nyumbani kwa msimu huu.

Mshambuliaji huyo mkataba wake unamalizika Juni mwakani, wakati ambapo atatimiza umri wa miaka 34, na bado hajakubali kusaini mkataba mpya na klabu hiyo.

Mechi yao ya mwisho ya LaLiga msimu huu ni dhidi ya Eibar ugenini, na pengine inaweza kuwa mara ya mwisho kwake kuvaa jezi ya Barca.

"Natumaini si tu kwenye mchezo dhidi ya (Celta) ameonyesha ubora wake, bado ni mchezaji bora duniani," alisema Koeman akiwaambia waandishi wa habari wakati alipoulizwa kama Messi amecheza mechi ya mwisho pale Camp Nou.

"Itakuwa ni ngumu kucheza bila yeye. Lakini Leo [Messi] yupo kivyake, kushinda zaidi na kupata pointi zaidi, tunahitaji wachezaji zaidi kufunga mabao.

"Leo [Messi] amefunga mabao 30 na amefanya tushinde pointi nyingi. Lakini majaliwa yake ni swali kwake.

"Kwa upande wangu mimi na klabu, tuna matumaini atabaki. Kwa sababu kama hakuna Leo, tunashaka kuhusu nani atafunga."

## TORRES AGOMBEWA MAN UNITED, NAPOLI

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United inaweza kukabiliwa na ushindani kutoka kwa Napoli kumsajili mlinzi wa kati wa Villarreal, Pau Torres, kwa mujibu wa Gazzetta dello Sport.

Mlinzi huyo wa Villarreal ameripotiwa kwamba, anatakiwa na miamba hao wa Ligi Kuu England, Man United, ambaye atacheza dhidi yao kwenye fainali ya Ligi ya Europa.

Lakini Napoli pia nao wanawania kumsajili mlinzi huyo wa kimataifa wa Hispania.

United inataka kuimarisha nafasi yake ya ulinzi, huku pia wakiwa wanahusishwa na mlinzi wa Real Madrid, Sergio Ramos na mchezaji mwenzake, Raphael Varane, pamoja na Jules Kounde wa Sevilla.

Torres anaonekana kuwa ndiye chaguo sahihi kwa Man United, ingawa Napoli nao wanamtaka kwa udi na uvumba kwa sababu bado hawajajua majaliwa ya nyota wao, Kalidou Koulibaly.

## DAVID LUIZ KUONDOKA ARSENAL

**LONDON, England**

MLINZI wa Arsenal, David Luiz ametoa taarifa kwamba, ataondoka ndani ya timu hiyo mwishoni mwa msimu huu.

Luiz alijiunga na Arsenal inayonolewa na Kocha Mkuu, Mikel Arteta kipindi cha majira ya joto mwaka 2019 akitokea Chelsea baada ya kukosa nafasi chini ya Frank Lampard.

Mlinzi huyo katika msimu wake wa kwanza ndani ya 'Washikabunduki, amepitia kipindi kigumu kutokana na kufanya makosa ambayo yaligharimu timu hiyo ikiwa




ni pamoja na mchezo wao dhidi ya Manchester City.

Licha ya makosa hayo, Arteta aliendelea kumwamini mpaka wakafanikiwa kutwaa Kombe la FA katika kikosi hicho.

Msimu huu hajawa na nafasi ya moja kwa moja ndani ya kikosi cha Arsenal kutokana na majeraha aliyopata kwenye mchezo dhidi ya Newcastle hivi karibuni.

Taarifa zinaeleza kuwa staa huyo ameomba kuondoka pale mkataba wake utakapoisha.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# ZIDANE: SIJAWAAGA WACHEZAJI MADRID

**Nawezaje kuwaambia naondoka kwa sasa? Mwishoni mwa msimu ndiyo tutaona nini...**

**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amekanusha ripoti kwamba amewaambia wachezaji wake anaondoka kwa miamba hao wa Hispania mwishoni mwa msimu huu.

Ripoti za awali zilidai kwamba, Mfaransa huyo amekijulisha kikosi chake wiki moja iliyopita kwamba, anaweza kuondoka mwishoni mwa msimu huu.

Zidane aliiongoza Real kushinda bao 1-0 dhidi ya Athletic Bilbao Jumapili, nakuwafanya wabakie kwenye mbio za ubingwa wa LaLiga hadi kwenye mechi za mwisho.

"Nawezaje kuwaambia wachezaji naondoka kwa sasa? Tunapambana kwa kila kitu ili kuwamo kwenye mbio za kuwania ubingwa," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Watu nje ya klabu wanaweza kusema vyovyote wanavyopenda, lakini mimi kwa upande wangu kamwe siwezi kuwaambia wachezaji wangu hivyo."

Real wamepitwa pointi mbili nyuma ya vinara Atletico Madrid, ambao walitoka nyuma na kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Osasuna nyumbani.

Kikosi cha Zidane kitacheza na Villarreal kwenye dimba la Bernabeu Jumapili ijayo wakijua kwamba, kama Atletico watapoteza au kutoka sare na Real Valladolid, wao wakishinda maana yake wametwaa taji.

"Mwishoni mwa msimu ndio tutaona nini kitatokea, lakini kwa sasa akili yetu ni kuangalia mchezo wetu wa mwisho," alisema Zidane.

"Hatuwezi kuendelea kuzungumza kuhusu majaliwa yangu ya baadaye. Mchezo wa mwisho kwa msimu ni muhimu zaidi kuliko hilo."

Zidane mwenye umri wa miaka 48, yupo katika kipindi chake cha pili cha ukocha hapo Real, mara ya kwanza akishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu mfululizo kati ya mwaka 2016 na 2018.

## KWA UFUPI

**WILLIAN KUONDOKA ARSENAL**

WINGA wa Brazil, Willian anatarajiwa kuondoka Arsenal mwishoni mwa msimu huu, lakini 'Washikabunduki' hao hawajapokea ofa yoyote kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32. ***(Fabrizio Romano, via Mail)***

**TIELEMANS, LEICESTER KUTETA**

KIUNGO wa kati wa Ubelgiji, Youri Tielemans, atafanya mazungumzo ya mkataba mpya na Leicester mwisho mwa msimu huu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ambaye alifunga bao katika fainali ya FA dhidi ya Chelsea, ana miaka miwili iliosalia katika mkataba wake. ***(Mail)***

**ALLEGRI KUMRITHI ZIDANE**

ALIYEKUWA Kocha wa Juventus, Massimiliano Allegri, anaonekana kuwa kipaumbele katika kuchukua nafasi ya Zinedine Zidane pale Real Madrid. ***(Marca)***

**XAVI ATAKIWA BARCELONA**

BARCELONA imeanza mazungumzo na kiungo wa kati wa zamani wa klabu hiyo, ambaye kwa sasa ni Kocha wa Al Saad ya Qatari, Xavi, kwenda kuchukua nafasi ya Ronald Koeman. ***(ARA Esports, via Football Transfers)***

**BOTMAN AITAMANI EPL**

MLINZI wa Uholanzi, Sven Botman mwenye umri wa miaka 21, ambaye alihusishwa na uhamisho wa kuelekea Liverpool Januari iliyopita, amesema Ligi Kuu England (EPL), ina kitu maalum.***(Athletic)***

**ALDERWEIRELD AWINDWA BRUGES**

BEKI wa Tottenham Hotspur, Toby Alderweireld analengwa na klabu ya Ubelgiji ya Club Bruges, lakini mchezaji huyo wa timu ya Taifa ya Ubelgiji hatafanya uamuzi kuhusu hatima yake hadi atakapojua ni nani atakayechukua nafasi ya ukocha. ***(Voetbal 24, via Express)***

**MURPHY AGOMBEWA EPL**

LEEDS United na Burnley wamejiunga na Southampton, Watford na Rangers katika mbio za kuwania kumsajili winga wa Newcastle United, Jacob Murphy mwenye umri wa miaka 26. ***(Football Insider)***

**PALACE WAMTAKA DRAGUSIN**

KLABU ya Crystal Palace inatumaini kumsajili mlinzi wa Romania mwenye umri wa miaka 19, Radu Dragusin kwa mkopo kutoka kwa klabu ya Juventus. ***(Sun)***

**CALHANOGLU NA HATIMA YAKE**

KIUNGO wa kati wa Uturuki, Hakan Calhanoglu ambaye mkataba wake unafikia mwishoni Juni pale AC Milan, amesema hatima yake haitegemei timu hiyo kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Sky Sport Italia, via Football Italia)***

**LOCATELI KUTOLEWA SOKONI**

MKURUGENZI wa Sasuolo, Giovanni Carnevali, amesema Manuel Locateli mwenye umri wa miaka 23, atabakia kwa klabu hiyo ya Serie A mwishoni mwa msimu huu, licha ya kuhusishwa na baadhi ya klabu. ***(Sky Sport Italia, via Football Italia)***



## HABARI MICHEZO

# UBINGWA SIMBA QUEENS BARA KAMA MUVI, WATUA MJENGONI

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

NI kama muvi ya kibabe! Ndivyo unavyoweza kusema kutokana namna Simba Queens ilivyotwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara huku watani zao, Yanga Princess wakisikilizia baada ya mechi yao kutangulia kumalizika juzi.

Katika mechi hizo za funga msimu zilizopigwa juzi, Simba ilikuwa ikiongoza kwa pointi 51 kabla ya mchezo wao dhidi ya Baobab uliochezwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, wakati Yanga ilikuwa na pointi 50 kabla ya kuikaribisha Alliance Girls kwenye dimba la Karume, Dar es Salaam.

Yanga Princess iliibuka na ushindi wa mabao 6-0 dakika chache kabla ya mchezo wa Simba Queens kumalizika wakati huo ikiwa haijafungana na Baobab, hivyo wadada hao wa Jangwani, kutega masikio yao wakianza kushangilia kuwa wametwaa ubingwa.

Milango katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri iliendelea kuwa migumu hadi dakika ya 90, lakini furaha ya Yanga ilibadilika ghafla na kuwa huzuni baada ya Asha Jaffar mchezaji raia wa Burundi kuipatia Simba bao pekee dakika za nyongeza na kuifanya timu hiyo kufikisha pointi 54 moja mbele ya watani wao.

Iwapo Simba ingetoka sare ingesalia na pointi 52 na Yanga Princess ingetwaa ubingwa kutokana na kuwa na pointi 53.

"Nawashukuru wachezaji wangu, viongozi na wadhamini wote ambao wametusapoti hadi kutwaa ubingwa. Tumefurahi. Ubingwa ulikuwa mgumu sana. Tumechukuwa ubingwa mara mbili mfululizo na tena bila kupoteza mechi yoyote," alisema Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi' mara baada ya mechi hiyo kumalizika.

Kwa upande wa Kocha wa Yanga Princess, Edna Lema, alisema: "Tunawapongeza Simba kwa kutwaa ubingwa. Tumejitahidi sana. Tumetoa upinzani mkubwa hadi mwisho wa mechi za ligi. Ni jambo la kujipongeza kwa sisi Yanga Princess kwani msimu uliopita tulishika nafasi ya saba, lakini safari hii tumeshika ya pili, ni jambo la kujipongeza.

"Naamini kilichotokea msimu huu kitaamsha ari mpya ya kutamani mafanikio makubwa, niwashukuru mashabiki wote wa Yanga kwa kipindi chote cha ligi kwa sapoti yao, wasiumie wala kukata tamaa waendelee kusapoti timu zao zote kwa wakati wote, hakuna nyakati za kudumu, itafika wakati furaha itarejea."

Wakati huo huo, wachezaji wa Simba Queens, jana walikaribishwa Bungeni jijini Dodoma.

"Shukrani kwa waheshimiwa wabunge wote ambao ni wana Simba, wakiongozwa na Mwenyekiti wao, Rashid Shangazi kwa kufanikisha Simba Queens kuwa timu ya kwanza ya wanawake Tanzania kuingia mjengoni," alisema Mgosi.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Jackson Group Sports, Kelvin Twissa (wa tatu kulia) akiwa katika picha ya pamoja na wadhamini mbalimbali baada ya kuzindua pambano la Rumble in Dar 2, ambalo bondia Hassan Mwakinyo atazichapa na Brendon Denes wa Zimbabwe Mei 28, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Next Door Arena, Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Pambano la Mwakinyo, Denes lapamba moto

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha mabondia wengi wanapata nafasi ya kuonyesha vipaji vyao, Kampuni ya Jackson Group Sports, imewapa nafasi zaidi mabondia wa Tanzania mbali ya bondia Hassan Mwakinyo, ambaye atazichapa na Mzimbabwe Brendon Denes kuwania mkanda wa uzito wa super welter wa Afrika (ABU) kwenye Ukumbi wa Next Door Arena, Mei 28, mwaka huu.

Awali, pambano hilo lilikuwa lishirikishe mabondia watatu tu wa Tanzania ambao ni Mwakinyo, Ibrahim Class na Shaban Jongo, hata hivyo, sasa watakaopanda ulingoni wameongezeka wanne zaidi kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Jackson Group Sports, Kelvin Twissa.

Mabondia hao ni Imani Daudi ambaye atazichapa na bondia wa Afrika Kusini, Chris Thompson, Hamis Palasungulu atakayezichapa na Ardi Ndembo wa Congo Brazzaville na mwanadada Halima Bandola akizichapa na bondia kutoka Bulgaria, Joana Nwamerue.

Pia katika orodha hiyo, yupo Daniel Materu ambaye naye atazichapa na bondia Pencho Tsvetkov wa Bulgaria.

Twissa amesema wameamua kufanya hivyo ili kukuza vipaji kwa mabondia wa Tanzania katika pambano hilo ambalo Benki ya KCB imetangaza kulidhamini kwa Sh. milioni 94.4.

Twissa amesema maandalizi ya pambano la raundi 12 yanaendelea vizuri na mkanda huo kwa sasa upo wazi.

Alisema siku hiyo kutakuwa na mapambano mengine makali ambapo bondia Jongo Jongo naye atawania ubingwa wa ABU dhidi ya Olanrewaju Durodora wa Nigeria huku Ibrahim Class akipanda ulingoni kumsindikiza Mwakinyo kwa kupambana na bondia Sibusiso Zingange kutoka Afrika Kusini.

"Hii ni sehemu ya pili ya Rumble In Dar na tunaitarajia kuwa kali na kusisimua kwani mabondia wanaopigana ni moto wa kuotea mbali," alisema Twissa.

Kwa upande wa Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya KCB, Christine Manyenye, alisema wameamua kutoa kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya pambano hilo ili kuendeleza mchango wao katika maendeleo ya michezo nchini.

## Vyuo vikuu waitaka wizara kuwageukia

**Na Idda Mushi, Morogoro**

WANAFUNZI wa vyuo vikuu vinavyomilikiwa na kanisa Katoliki nchini wameishauri serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuiendeleza sekta ya michezo kwa wanafunzi wa elimu juu badala ya kuishia ngazi ya elimu za msingi na sekondari pekee.

Wakizungumza mjini Morogoro katika Bonanza la Vyuo Vikuu vinavyomilikiwa na kanisa Katoliki nchini, wanafunzi hao walisema hatua hiyo itasaidia kukuza na kuendeleza vipaji vya wanafunzi wa elimu ya juu waliopo vyuoni.

Mratibu wa bonanza hilo, ambaye ni Katibu wa Kamati ya Maandalizi, Michael Luoga, alisema miongoni mwa michezo inayochezwa zaidi chuoni ni pamoja na mpira wa miguu, mpira wa pete pamoja na mpira wa wavu ambayo pia ilikuwamo katika bonanza hilo lililoshirikisha vyuo vitano vya Kanisa Katoliki.

Baadhi ya wanafunzi walioshiriki bonanza hilo lililoanza Jumamosi na kumalizika jana, Ilmala Nungu na Joseph Jafary, waliitaka serikali na wadau wengine wa michezo kutembelea mashindano mbalimbali yanayoendeshwa vyuoni kama njia mojawapo ya kuibua vipaji kwani kupitia huko ni rahisi kupata wanamichezo wenye kujitambua watakaowakilisha vyema taifa katika michezo ya aina mbalimbali.

"Mfano chama cha soka, kinaweza kutuma wataalamu wake kupita kukagua mashindano ya mpira wa miguu, vivyo hivyo chama cha mpira wa pete na vyama vingine, nina uhakika vyuoni kuna wachezaji wazuri wenye uwezo wa kuipaisha nchi kitaifa na kimataifa," alisema Nungu.

## JKT Tanzania yapania tatu za Yanga kesho

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI kikosi chao kikiendelea kujifua kuelekea mechi ya kesho dhidi ya Yanga, itakayopigwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, Msemaji wa timu hiyo, Jamila Mutabazi, amesema kwa mujibu wa Kocha Mkuu, Muhamed Abdallah Bares, morali ya wachezaji wao upo juu tayari kupambania pointi tatu.

"Japokuwa tunakutana na timu ambayo inashikilia nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu, kocha amesema haihofii kwa sababu tumejipanga vizuri kuhakikisha hatupotezi mchezo huo," alisema Jamila.

Alisema mchezo huo unatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa kutokana na maandalizi yaliyofanywa na kila timu huku akiwaomba mashabiki wao wajitokeze kwa wingi uwanjani ili kuwapa hamasa wachezaji waweze kutimiza mipango yao.

# Michezo

Jumanne Mei 18, 2021

Nipashe




ZIDANE: SIJAWAAGA WACHEZAJI MADRID

HABARI UK 22

MWOKOZI...



Kipa wa Liverpool, Alisson Becker, akiunganisha nyavuni mpira wa kona kwa kichwa na kuipa timu yake bao la ushindi dakika za majeruhi wakati ikishinda 2-1 dhidi ya West Bromwich Albion, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa The Hawthorns juzi. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA: TUTAISHANGAZA DUNIA MATOKEO KAIZER

●●●Wawaita mashabiki kwa Mkapa, kuingia kambini leo, Morrison naye asema...

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha wawakilishi wa Tanzania kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, kimetua jijini Dar es Salaam jana kikitokea Afrika Kusini baada ya mechi yao ya mkondo wa kwanza ya robo fainali ya michuano hiyo dhidi ya Kaizer Chiefs, na kueleza "tutaishangaza dunia" katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi.

Simba ilikubali kipigo cha mabao 4-0 kutoka kwa Kaizer Chiefs kwenye mechi hiyo ya robo fainali ya kwanza iliyopigwa Uwanja wa FNB nchini humo Jumamosi iliyopita, hivyo inahitaji ushindi kuanzia mabao 5-0 ili kutinga nusu fainali.

Lakini Mratibu wa klabu hiyo, Abbas Ally, amewatoa hofu mashabiki wa timu hiyo kwa kuwataka kuendelea kuisapoti timu wakati wote kwa kuwa kama wao waliweza kuwafunga kwao hata Simba inaweza kushinda nyumbani.

"Mpira mara nyingine una matokeo ya kikatili, lakini tunawaomba mashabiki wetu ambao wamekuwa wakitusapoti muda wote bila kujali matokeo waendelee kutusapoti, tutaishangaza dunia kwa kile ambacho tutakwenda kukifanya hapa.

"Tunaenda kuanza maandalizi, kama wao waliweza kutufunga kwao na sisi tunaweza kuwafunga kwetu. Kama CAF (Shirikisho la Soka barani Afrika), itatupa nafasi ya mashabiki kuingia uwanjani, waje kwa wingi Jumamosi kutusapoti.

"Tunapofungwa na kushinda wamekuwa pamoja nasi, kile walichokifanya wazee wetu miaka ya 75 tunakwenda kukirudia," alisema.

Abbas alisema Simba si timu ya kwanza kufungwa mabao manne na kufafanua kuwa hata Brazil iliwahi kukutana na kipigo kikali cha mabao saba kwenye Kombe la Dunia, hivyo Simba kufungwa si kitu cha ajabu.

Kwa upande wa Ofisa Habari wa klabu hiyo, Haji Manara, alisema: "Hatuna majeruhi yeyote, tumewapa wachezaji mapumziko ya siku moja na kesho [leo] jioni wataingia kambini kuanza maandalizi ya mechi ya marudiano, kesho [leo], tunazunguza zaidi na waandishi wa habari."

Kwa upande wa Kocha Mkuu, Mfaransa Didier Gomes, tayari alishaeleza: "Jambo lolote linawezekana kwenye mpira, hatujafurahia matokeo lakini bado tuna matumaini, ni muhimu sana kuamini kwamba tunaweza kubadili matokeo. Lakini kama tunataka kupata matokeo mazuri kwenye mchezo wa marudiano lazima tuwe bora zaidi."

Wakati huo huo, winga wa timu hiyo, Mghana Bernard Morrison, ambaye hakusafiri na timu yeye ametuma ujumbe kupitia mtandao wake wa Twitter akieleza: "Wakati shujaa anapojikwaa, waoga hufurahi. Hakuna anayehisi vizuri kwa mwoga kuliko kuona mtu mzuri akianguka. Wakati wanasema huwezi kufanya, waambie wakae chini na kuangalie jinsi unavyofanya."

Katika michuano hiyo hatua ya awali mwaka 1979, Simba ilikubali kipigo cha mabao 4-0 nyumbani dhidi ya Mufulira Wanderers FC ya Zambia na ilipokwenda ugenini ikapindua 'meza' kwa kushinda 5-0 na kusonga mbele.

## YANGA, SIMBA ZATOA NENO KUVAANA JULAI

**Na Saada Akida**

WAKATI mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara, ambayo ilishindwa kuchezwa Mei 8, sasa ikipangwa kupigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Julai 3, mwaka huu, viongozi wa klabu hizo kongwe nchini wametoa neno.

Timu hizo katika raundi ya kwanza zilitoka sare ya bao 1-1 na mchezo wa raundi ya pili uliotakiwa kuchezwa Mei 8, haukufanyika kutokana na Yanga kugomea kucheza saa 1:00 usiku baada ya taarifa kutoka Shirikisho la Soka nchini (TFF) kusogeza muda huo kutoka saa 11:00 jioni muda wa awali, kwa kile ilichoeleza ni maagizo kutoka serikalini.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa juzi na Bodi ya Ligi nchini (TPLB), inaonyesha mchezo huo utachezwa saa 11:00 jioni kama ilivyokuwa awali.

Kwa upande wa Yanga kupitia Mkurugenzi wa mashindano, Thabiti Kandoro, amesema kikosi chao kipo tayari kukutana na timu yoyote kwa sababu wana kikosi imara cha kuweza kukutana na kupata matokeo mazuri dhidi ya Simba.

**"Tuko tayari kucheza mechi hiyo na matumaini makubwa ya kufanya vizuri kwa sababu tumeona mabadiliko katika kikosi, hivyo nina imani kubwa ya kupata matokeo mazuri katika mchezo huo dhidi ya Simba," alisema Kandoro.**

Naye Mkurugenzi wa mashindano ya Simba, Hamisi Kisiwa, alisema hawana presha na ratiba hiyo kwa sababu msimu huu wamejipanga kutetea mataji yao ikiwamo kutetea ubingwa huo kwa kushinda mechi zao zote ikiwamo dhidi ya Yanga.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002